

# Vita Vikuu Sana Vilivyowahi Kupiganwa

Jeffersonville, Indiana, USA

Machi 11, 1962

1 Asante, Ndugu Orman. Bwana akubariki.

Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha kuwepo hapa tena asubuhi hii, na kwa namna fulani kidogo nadhani sikulitazamia, nami nina hakika isingetazamiwa na kusanyiko. Nami nilikuwa tu nikisoma na ... Asante, dada. Na Bwana alionekana tu kuweka kitu fulani kidogo moyoni mwangu, kukileta Kanisani, nami nilifikiri ilikuwa ni wakati wa kufanya jambo hilo. Na sasa hii ...

Nilipofika, halafu bila kujua tutakuwa hapa Jumapili hii, nimetangaza ya kwamba nina U—Ujumbe kwa ajili ya Kanisa. Nami ninataka, Mungu akipenda, kuleta Ujumbe huu Jumapili ijayo. Na kutakuwako na muda mrefu sana, kwa hiyo, labda hautatoka kabla ya saa sita na nusu, saa saba, labda, kama wakati huo. Umekuwa moyoni mwangu kwa muda mrefu, nami nafikiri nadaiwa na watu jibu kwa nini sikuwa na juhudi huko nje. Nimehubiri kote kote, lakini nina hakika kamwe haikufikia mahali inapopaswa kuwa. Kwa hiyo nafikiri, Bwana akipenda, Jumapili ijayo, ninataka tu kuchukua muda wangu na kueleza tu, sababu yake na kwa nini, na kuwaonesha kimaandiko yanayoendelea, mnaona, kuwaeleza tu kwa nini haya yote. Kwa sababu, labda nitakuwa ninaenda nje ya nchi ama mahali fulani mara moja. Ninangojea sasa kuona ni wapi Yeye ataniita niende. Mwisho ...

2 Yapata usiku wa siku tatu au mbili zilizopita, nilipata simu karibu na usiku wa manane, na ilikuwa kwa ajili ya kumwomba mwanamke fulani aliyekuwa hospitalini. Nao wakanipigia simu, na kusema, "Omba." Nami ninasahau jina walilonipa, kwamba ... Wakasema alikuwa rafiki wa Bibi James Bell, dada yetu hapa kanisani, dada mweusi, mwanamke mwaminifu, mzuri sana. Naamini jina hilo lilikuwa ni Shepherd, nililopewa. Kwa hiyo nikatoka kitandani na kupiga magoti, na—na kumwambia mke wangu. Simu ilipolia, ilimwamsha. Nami nikasema, "Hatuna budi kumwomba Bibi Shepherd, dada ambaye alipiga simu ambaye ni rafiki wa Bibi James Bell." Kwa hiyo tukamwomba, tukarudi kitandani.

3 Na halafu kwenye yapata saa nne ama saa tano, kesho yake, nikapigiwa simu tena. Ilikuwa ni Billy. Naye akasema, hakuwa Bibi Shepherd, alisema alikuwa ni Bibi Bell, mwenyewe, si rafiki wa Bibi Bell. "Ilikuwa ni Bibi Bell, naye yuko hospitalini mahututi." Na nilipokimbia kwenda kule hospitalini, tayari alikuwa ameaga dunia. Bwana alikuwa amemwita Bibi Bell, Nyumbani.

4 Bibi Bell alikuwa mshiriki mwaminifu pamoja nasi hapa kanisani kwa miaka mingi. Mumewe, mimi na mumewe, James, tulifanya kazi pamoja, na baba yangu, miaka mingi iliyopita, nje, huko kuendesha ... Kuvileta hivi vichokoo, kutoka Pennsylvania, hadi hapa Colgate, miaka mingi iliyopita, nadhani miaka thelathini iliyopita, ama zaidi. Nasi tunampenda Dada Bell. Alikuwa mtu mwenye heshima.

5 Nami nafahamu alishikwa na ugonjwa mbaya wa kibofu cha nyongo, na hao ... Daktari wake, aliyejua ugonjwa ule vizuri sana, alikuwa nje ya mji wakati ule. Ndipo daktari mpya akaja kumwangualia, na—na akashauri upasuaji wa dharura, naye hakuishi. Na—naye alikuwa ... Nafikiri yeye ... Ninavyofahamu mimi, ni kwamba daktari wake wa sikuzote asingeagiza huo—huo upasuaji, kwa sababu alikuwa mnene, na kibofu chake cha nyongo kilikuwa kibaya. Naye alikuwa na mawe, nafikiri, ama kitu fulani ndani yake, na —na Bwana alikuwa amemrehemu. Alikuwa amepata mashambulio hayo hapo kabla na Bwana alikuwa ameshughulikia hayo, mara nyingi. Bali ikawa tu kwamba... Vema, kama tukilileta kwenye kipimo kamili, tugesema hivi; Mungu amemwita Dada Bell, na hivyo ndivyo inavyopaswa kuchukuliwa, mnaona.

6 Na jinsi ambavyo alikosea, alilileta hilo kwangu, kwamba nilifikiri ilikuwa Bibi—Binti Shepherd. Sikumjua Binti Shepherd. Binti huyo huenda akawa hapa, asubuhi hii, nami huenda nikamjua kama nikimwangualia usoni. Bali, ilisemwa ilikuwa Bibi Shepherd. Na kama yote yalifanywa namna hiyo, ili kwamba kama ... Kama ninngejua ilikuwa Bibi Bell alikuwa katika hali hiyo, labda ningekwenda huko na kuanza kumwomba moja kwa moja. Na halafu, mnaona, ya kwamba, Mungu hakutaka tufanye jambo hilo, labda. Kwa hiyo, "Tunajua ya kwamba mambo haya yote hutenda kazi pamoja kwa ajili ya kuwapatia mema wale wampendao Mungu."

7 Nami nina hakika ya kwamba Dada Bell alimpenda Bwana wetu. Alikuwa mwanamke mzuri. Sasa, yeye ni mmoja wetu. Ndani hapa, hatuna mipaka yo yote ya rangi. Familia ya Mungu haiweki mipaka ya rangi. Kama tu wekundu, kahawia, weusi, au manjano haijalishi, weupe. Hata iwe nini, tu ndugu na dada katika Kristo Na kwa hiyo tu—tunampenda. Nasi tutamkosa, sisi wa maskani haya. Jinsi nitakavyozikosa, hizo "amina" kubwa mno, za sauti yenye mikwaruzo nyuma kule pembeni, za Dada Bell. Na katika kumpeleka nyumbani, angezungumzia kuhusu Bwana Yesu.

Na kama ninalielewa vizuri, sikujua hilo mpaka tu muda mfupi uliopita, bali nafikiri mazishi yake yatakuwa papa hapa kanisani. [Ndugu Neville anasema, "Hiyo ni kweli." — Mh.] Jumanne hii ijayo kwenye ["Saa saba kamili."] Saa saba kamili. Nafikiri mimi na wewe yatubidi tushiriki rasmi ["Hiyo ni kweli."] katika ibada hii ya mazishi.

8 Bali, katika kusanyiko, kwa kuwa tumepungua nguvu kwa mmoja asubuhi hii. Kwa heshima ya Dada yetu Bell, hebu na tusimame kwa miguu yetu kwa muda kidogo tu, tunapoinamisha vichwa vyetu.

Mungu wa uzima, Ambaye unatoa na kuuchukua uhai, kama Ayubu wa kale alivyosema, “Bwana hutoa na Bwana hutwaa; Jina la Bwana libarikiwe.” Miaka michache iliyopita, Wewe ulimtuma Dada Bell miongoni wetu, awe raia mwenzetu pamoja nasi, wa Jumua kuu ya Mungu. Nasi tunakushukuru kwa kila uvuvio aliokuwa nao kwetu, jinsi ambavyo alipenda kuimba, na kushuhudia, na angejazwa sana na Roho mpaka angepiga kelele na kupaza sauti. Na hakuonea haya Injili ya Yesu Kristo, kwani kwake Hiyo ilikuwa nguvu ya Mungu kwa wokovu. Kuona miaka yake imehesabiwa, na saa yaja wakati sote yatupasa kujibu. Na Wewe umemwondoa kwetu, asubuhi hii, apate kuwa katika Uwepo Wako. Kwa kuwa, ni kweli kwamba, tunapoondoka hapa, tuko katika Uwepo wa Mungu.

9 Ee Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya yote. Tunaomba ya kwamba utambariki mumewe, rafiki yangu, James; mwanawe, binti zake, hao wote. Tunafahamu ya kwamba mvulana wake anaruka kutoka Ujerumani, kutoka kwenye jeshi, kuja nyumbani, kutoa heshima za mwisho awezazo, duniani, kwa mama yake aliyeaga dunia. Jinsi hapana budi moyo wa kijana yule unapigapiga asubuhi hii. Ninamwomba, Bwana. Mungu, mbariki. Mbariki Jimmy, na jinsi alivyo ... Kumwona akifanya kazi huko nje, na masaa ya uchovu, kupata riziki kwa ajili ya jamaa yake. Ninaomba ya kwamba jamaa hiyo kuu haitatenganishwa, bali gurudumu la familia halitavunjwa katika ile Nchi upande ule mwingine.

Hebu sisi, Bwana, sasa tukaze silaha zetu na ule mshipi ukazwe zaidi, na kutoka kwenda vitani sasa, kupigana huku tumepungukiwa na mtu mmoja kuliko tulivyokuwa juma lililopita. Tunaomba kwamba Wewe utatuhifadhi, na kutuimarisha, na kutusaidia tunapoendelea, na siku moja sote na tukusanyike pamoja tena kule ng'ambo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

10 Sasa, roho ya dada yetu aliyeaga dunia na ikae katika amani. Ningetaka kusema ya kwamba ma—mazishi yake yatahubiriwa hapa Jumapili, ama Jumanne, nasi tunge- ... Mtu ye yote anayeweza kuyahudhuria amekaribishwa. Nadhani Ndugu Neville hapa ana taratibu. [Ndugu Neville anathibitisha — Mh.] Nawe ulikuwa nao. Sasa, leo, ninaninii tu ...

11 Mnaona, hakuna wengi sana. Kama kungeweza kuwa na kiti mahali fulani kiletwe kwa ajili ya Ndugu na Dada Slaughter nyuma kule. Nilipata simu yako, Dada Slaughter, na nikaenda kumwomba ninii—yule Dada Slaughter mwingine, Dada Jean Slaughter aliye na homa ya sungura, tularemia. Yeye kweli ni mahututi, bali tunamtumaini Mungu kwamba atakuwa mzima.

12 Sasa tunataka kusoma Maandiko fulani. Nami nataka tu kufundisha asubuhi hii, nikichukua wakati wangu, sababu tangu niliporudi kutoka Arizona, vema, koo langu lina maumivu kidogo.

Na sasa, Jumapili ijayo msisahau, na nafikiri Billy tayari amekwisha peleka yale—yale matangazo Na itakuwa ni ibada ndefu kabisa, tunaamini, kwa hiyo njoni mapema mwezavyo. Tunataka kuanza, yapata saa tatu na nusu, ama ninamaanisha, saa nne. Na huenda ikawa, kumbukeni, yapata saa saba ama saba ... labda, au saa sita na nusu, saa saba, kitu kama hicho, saa tatu ama nne, au zaidi, ningetaka kuchukua, na kuchukua tu Maandiko. Leteni penseli zenu na karatasi, na myaandike. Kukiweko na swali lo lote, liulize—liulize, mnaona, na labda twaweza kulielezea, kufanya tuwezalo kusaidia.

13 Sasa hebu na tusome baadhi ya Maandiko, kwanza, sasa. Nina sehemu tatu katika Biblia, ambazo ningetaka kusoma. Na ya kwanza, kama unataka kuiandika, na iwapo una penseli, nataka kurejea asubuhi hii, kwenye vifungu vingi ambavyo ninge ... ama Maandiko mengi, hasa, ambayo ningetaka kuyarejea. La kwanza litakuwa I Petro 5:8-10, Waefeso 6:10-17, na Danieli 12:1-14. Sasa, katika kusoma, tukichukua wakati wetu.

14 Na kila mtu karibu ameketi. Kwa hiyo, wachache bado wamesimama, huko nyuma na pembeni. Lakini tutajaribu kumaliza haraka iwezekanavyo na kuwaachilia mtoke, ndipo tutawaomba wagonjwa.

Tuna maskini mama anayelala hapa asubuhi ya leo, ambaye ni mgonjwa sana. Ninafahamu ya kwamba alikuwa mgonjwa sana, jana. Na mimi—nami nilitaka tu asikize asubuhi hii kwanza kabla sijamwomba. Nami ninajua hali za maskini mama huyo. Naye ni mahututi, bali tunaye Baba yetu mkuu sana wa mbinguni Ambaye ameshinda kabisa maradhi yote. Nami nina ninii—kidogo ...

15 Nalimsihi Bibi Wood kama angeisoma, lakini yeye—yeye alisita kidogo ku—kufanya hivyo. Makala fulani, ambapo daktari wa utabibu hakika alishangazwa. Wakati, yeye alipokuwa mkosoaji juu ya uponyaji wa Kiungu na hata asingemruhusu mtu ye yote kuzungumzia jambo hilo ofisini mwake; na nesi wake, pia. Kwa hiyo ilitokea kwamba, alipata mgonjwa ambaye alikuwa na ugonjwa wa saratani—saratani kubwa. Hakutaka kujihusisha nayo, kwa hiyo akampeleka kwenye hospitali nyingine. Hawakutaka uhusiano wowote na jambo hilo kule, kwa hiyo wakamrudisha. Kwa hiyo wao ... Loo, ilikuwa kwenye kifua, na ilikuwa katika hali mbaya sana. Na ngozi yote ilikuwa imeliwa. Na hiyo saratani, ikashuka ikaingia kwenye matiti, ikaingia kwenye mbavu. Nadhani mnafahamu ninaloamaanisha.

16 Wao wana rafiki yetu daktari mdogo kutoka Norway ameketi pamoja nasi asubuhi ya leo.

Naye alitayarisha vyombo vyake vyote, kwa maana alisema alijua kwamba—kwamba yule bibi alimtaka amfanyie upasuaji na aondoe lile titi. Nayo ilikuwa kazi yenye damu nyingi sana. Na—naye

akatwaa vifurushi vyake vyote, kila kitu. Yule nesi alimtayarisha bibi huyo na kumleta katika chumba cha upasuaji, kisha akarudi kuchukua vyombo, pia, ambavyo vingelazimika kutumiwa na daktari na msaidizi wake, kutoa titi. Na kwa hiyo walikuwa na taulo na kadhalika. Na kwa hiyo wakaanza ...

17 Wakati alipoanza kugeuka, mumewe alitaka kujua kama angeweza kuketi mwishoni mwa chumba na kuomba. Yeye alikuwa mhubiri wa utakatifu. Naye akaketi pale kando ya mguu wa kitanda, na kuomba. Bila shaka, daktari hakuridhika sana na jambo hilo, mwajua, yeye akiwa mle ndani. Lakini mradi tu asingengalia, wala isingemdhuru, mbona, "Nadhani ilikuwa ni sawa; hange—hangezimia."

18 Kwa hiyo wakati akiwa ameketi, anaomba, kukaja kupigapiga mabawa kwenye kile chumba. Naye daktari anageuka aende, pia, akiwa na vyombo vyake kuanza kuondoa lile titi. Alisogea vifaa baada ya vifaa. Hata hakukuwa na kovu kwenye titi; hakuna hata kovu. Yeye alisema, "Ninii—ninii ... Je, inahama?" Naye akaanza ... Na nesi huyo alitoa ushuhuda wake. Wote wawili wametoka na wamekuwa wapentekoste, wamejazwa na Roho Mtakatifu, wakimtumikia Bwana. Hakuna hata kovu!

19 Daktari Holbrook alishuhudia, mwenyewe, akasema, "Dakika moja kabla ya hapo, kulikuwepo yule—yule mwanamke amelala pale, na yule nesi, huku kansa kubwa mno imetokeza yote kwenye titi lake; Na dakika moja baadaye, hapakuwa hata na kovu ambapo ilikuwa imeondolewa." Huyo ni mmoja wa madaktari wetu wazuri wa matibabu hapa Marekani. Yeye alisema alikuwa ameshawishika papo hapo. Na yeye, hata hivyo, alikuwa shemasi katika kanisa. Mnaona?

Mnaona, watu hufikiri kanisa ni mahali tu unapokwenda tu na ni, "Loo, unaenda mle kujifunza kuwa mzuri, ama jambo kama hilo." Sivyo ilivyo, , rafiki. La. Mungu ni Mungu. Yeye ni mkuu leo kama alivyokuwa, aliyepata kuwa. Naye daima atakuwa yule yule. Naye ni ninii ... Tunampenda tu.

20 Sasa, tunataka kusoma sasa kutoka 1 Petro, sura ya 5, aya ya 8 na ya 10, kwanza.

*Mwe na kiasi...na kukesha; kwa kuwa mshtaki wenu ibilisi,...simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze:*

*Nanyi mpingeni huyo, kwa uthabiti...katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.*

*Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Yesu Kristo, ninyi mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, awathibitisha, awatie nguvu, na kuwaimarisha.*

21 Mungu asifiwe iliyoje! Sasa katika Kitabu cha Waefeso. Tungependa kufungua hapa kwenye Kitabu cha Waefeso sura ya 6, na tungetaka kusoma toka aya ya 10 hadi ya 17 ambapo nimetia alama.

*Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uweza wa nguvu zake.*

*Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.*

*Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza la dunia—la dunia hii, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*

*Kwa sababu hiyo twaeni binafsi silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushinda siku ya uovu,...mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.*

*Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni,...na kuvaa dirii ya haki kifuani;*

*Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;*

*Zaidi ya yote, ... mkitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.*

*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu:*

22 Sasa katika Kitabu cha Danieli, ningetaka kusoma mengine zaidi. Sasa, Danieli sura ya 12. Ninataka kuanza kwenye ya 1 na kusoma se—sehemu ndefu kabisa ya hii, aya kumi na nne.

*Wakati huo...Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa...wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.*

*Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele,...wengine aibu na kudharauliwa milele.*

*Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao wageuzao—wageuzao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele.*

*Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge—yafunge...kitabu, hata wakati wa mwisho: wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.*

*Ndipo mimi, Danieli, nikatazama, na kumbe, wamesimama wengine wawili,...mmoja ukingoni mwa mto upande huu, na mmoja ukingoni mwa—mto upande wa pili.*

*Na mmoja akamwuliza yule mtu aliyevikwa nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, Je! itakuwa muda wa miaka mingapi hata mwisho wa mambo haya ... ya ajabu?*

*Nami nikamsikia yule mtu aliyevikwa nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, hapo alipoinua mkono wake wa kuume na mkono wake wa kushoto kuelekea mbinguni; akaapa kwa yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba itakuwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati; tena watakapokuwa wamekwisha kuvunja nguvu za hao watu watakatifu,...mambo hayo yote yatakapotimizwa.*

23 Ninaamini nitakoma papa hapa. Ninataka kuchukua fungu la maneno, kama lingelitwa somo kutoka hapo, kutokana na hilo, kutoa hitimisho hili la: *Vita Vikuu Sana Vilivyowahi Kupiganwa*. Hayo ndiyo ninayotaka kutumia kwa ajili ya somo.

24 Sasa, jinsi nimelipata hili kwa ajili ya somo la asubuhi hii. Tumerudi tu; baadhi ya wadhamini, hapa kanisani, na mimi mwenyewe, tulikuwa huko Arizona. Nasi tulitoka, kwenda kule hasa, kufanya mkutano hapo Phoenix, na Ndugu Sharrit, kwenye maskani yake. Lakini nilipoona kwamba ndu—ndugu fulani alikuwa mjini, akifanya ibada katika hema, vema basi, nilijisikia kidogo sipendelei kufanya mkutano. Niliwazia kwamba labda nitaufanya Jumapili alasiri, kusudi asiudhiwe mtu ye yote katika makanisa yao. Lakini, nikaona, ya kwamba alikuwa na ibada za Jumapili alasiri, pia. Nami nilikuwa na—na wasiwasi kidogo kuhusu kufanya ibada.

Na hivyo sisi ndugu, badala ya kuendelea siku nzima, kwa vile tulikuwa tumetoka kwenda kuwinda, tulienda mjini, tukaendelea na kujiandaa, na tukaenda kwenye ibada za Ndugu Allen. Ndugu A. A. Allen alikuwa akifanya ibada. Kwa hiyo tukaenda kwenye ibada, na Ndugu Allen akahubiri mahubiri makuu. Tulikuwa na—na wakati, wakati mzuri tukimsikiliza Ndugu Allen, kusikia wa—waimbaji, na kadhalika, jinsi walivyoimba, na kupaaza sauti, na tukawa na ibada nzuri sana.

25 Ndipo tukaona, kote barabarani, mkono wa Bwana. Popote tulipoenda, Bwana Yesu angekutana nasi. Na kuna jambo fulani kuhusu kuwa peke yako, huko nje jangwani. Kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo, kwamba kama ukiwa peke yako namna hiyo, kuna kitu kinachokuvuta. Hiyo ni, nadhani, ndiyo sababu moja ninapenda sehemu hizo za nje. Unaondoka kwenye nguvu za adui, kadiri tulivyo nazo hapa.

26 Ibilisi karibu hana madhara isipokuwa anaweza kuwa na kitu cha kutendea kazi ndani yake, awenacho. Mnakumbuka wale pepo waliotolewa katika Jeshi, walikuwa nacho? Wanataka kufanya madhara zaidi, kwa hiyo walitaka kwenda kuwaingia wale nguruwe. Kwa hiyo pepo yabidi wapate kitu fulani cha kutendea kazi, mtu watakayemtumia.

Na hivyo ndivyo Mungu anavyofanya, pia. Hana budi kuwa na sisi. Yeye anatutegemea sisi kutenda kazi kwa sisi.

27 Na wengi walikuja tulipokuwa safarini, wakiwa na ndoto. Na Bwana Yesu hakushindwa kamwe bali alitoa tafsiri sahihi, na ikawa tu, sawa kabisa.

Ndipo basi Yeye alikuwa mwema kwetu, akatuongoza kwenye wanyama na kutuambia walipokuwa. Na, wajua, kuwa tu karibu nasi jinsi hiyo, ni la ajabu tu. Tukaketim, usiku kucha, kwenye moto wa kambi, mbali na kila mtu, kwa maili kadha wa kadha, na kuangalia ule—ule moto wa kambi wenye kusinzia kwenye mizingo ya miamba Na loo, ilikuwa ajabu kwelikweli!

28 Ndugu mmoja pale, aliyekuwa na shida na mkewe, ambaye alikuwa ... Miaka mingi iliyopita, aliinua kichwa chake kwenye mkutano, ambapo nilikuwa nikifanya ibada. Nami nilikuwa nimewaomba wainamishe vichwa vyao; kulikuwa na pepo mchafu ambaye asingemtoka mwa—mwanamke, jukwaani. Naye mama huyo, bila kicho tu, akainua kichwa chake hata hivyo. Ndipo huyo roho akamwacha yule mwanamke, jukwaani, akaenda kwake. Na hii ni karibu miaka kumi na minne, na mama huyo amekuwa katika hali mbaya; sana, hata akaingia kichaa, mpaka anafanya mambo yasiyofaa. Kwa mfano, alimwacha mumewe akaenda akaolewa na mwanamume mwingine huku anaishi na mumewe; akadai hakujua amefanya hivyo. Na kwa hiyo wao—wao walijaribu kumchunguza kwa ajili ya jambo hili. Je, unasema hicho kitu gani, wakati wewe ... Usahaulifu? Ni ... Jamani, sijui jina hilo. Nadhani hiyo ni kweli, daktari. Lakini haikuwa hivyo. Ilikuwa ni roho. Naye ... Naye mama huyo alikuwa ni rafiki yangu mzuri. Lakini tangu usiku huo, na kuendelea, alinichukia makusudi. Bila shaka, unaweza kuona sababu yake.

29 Lakini basi wakati mumewe alipokuja, nasi tulipiga magoti chumbani kuomba, ndipo Roho Mtakatifu akashuka. Mambo yakaisha. Ndipo akamtokea mumewe usiku huo, katika ndoto. Alirudi na ndoto, alidhani ilikuwa ni mzaha. Nikaja kuona, lilikuwa ndilo jibu hasa la uponyaji wa mkewe. Jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alitenda kazi!

Na kuendelea huko Tucson, pamoja na Ndugu Norman na hao wengine, na hapo Bwana akaanza kufanya kazi tena kwa mambo makuu, yenye nguvu na kufunua mambo.

Usiku mmoja, kilichonivuta kwenye hitimisho hili hapa, nilikuwa nimesimama pamoja na Ndugu Wood na Ndugu Sothmann. Nasi tulikuwa ... Ilikuwa yapata saa nne usiku, nami nilikuwa nikiangalia juu angani, na hofu kuu ikanijia. Nami nikasema, "Angalia tu! Majeshi hayo yote makubwa, ya mbinguni!" Nami nikasema, "Kila kitu kimepatana kikamilifu."

30 Naye Ndugu Wood akasema, "Ukiangalia nyota ndogo mbili zinazokaribiana sana hata, inafanya zinaonekana kama nuru moja."

31 Nikasema, "Lakini, unajua, Ndugu Wood, kulingana na sayansi, katika hilo kundi la nyota saba, lile kundi dogo, lile kundi kubwa, hizo nyota hazionekani ziko umbali wa inchi mbili kati yao; nazo ziko mbali zaidi zenyewe kwa zenyewe kuliko sisi tulivyo mbali nazo. Na kama zingeanza kuja huku duniani, zingechukua, katika mwendo wa maili elfu kadhaa kwa saa, ingelichukua mamia na mamia ya miaka kwa hizo kufika duniani." Nami nikasema, "Katika utaratibu wote huu mkubwa, mfumo mno hapa, na isitoshe wanatuambia wanaangalia kwa darubini, wanaweza kuona muda wa miaka milioni 120 ya nuru, huko mbali sana; na bado kuna miezi na nyota. Na—na, hata hivyo, Mungu aliumba kila moja ya hizo. Naye anaketi katikati yazo."

32 Nami nikasema, "Mahali fulani ndani mle nilipoonyeshwa, wakati fulani katika kituo cha uchunguzi, ile zodiaki; huanza na bikira, ikaja juu kupitia wakati wa kansa, na kuendelea chini mpaka la mwisho lilikuwa ni simba, Leo yule Simba. Kuja mara ya kwanza kwa Kristo ilikuwa ni bikira; kuja mara ya pili, kwa Simba wa kabila la Yuda." Nami nikasema, "Nimejaribu niwezavyo kuona hiyo zodiaka, nami siwezi kuona. Lakini, hata hivyo, imo mle. Wale waliofunzwa, wanajua imo. Ayubu aliiona. Watu walizoea kuiangalia. Ilikuwa ni Biblia, siku moja. Bali katika kusanyiko lote lile la mamilioni na mabilioni ya muda wa miaka ya nuru, Mungu huketi kati ya hizo zote, Naye anatazama chini. Paulo yuko mle ndani. Mama yangu yuko mle ndani, mahali fulani, akiangalia chini."

33 Na niliwaza kuhusu utaratibu wa lile jeshi la mbinguni, hakuna mmoja wao aliye nje ya mahali pake. Kila mmoja hushika majira yake, kikamilifu, Jeshi kuu la Mungu! Niliwaza kuhusu askari, jinsi ambavyo kama mwezi ule ungeondoka kwenye utaratibu, dunia ingefunikwa tena na maji, katika dakika chache tu. Dunia ingekuwa tu kama ilivyokuwa wakati Mungu alipoamua kuitumia, kutuweka sisi hapa juu yake. Ilikuwa ukiwa, tena tupu, na giza, na maji yalikuwa yametapakaa juu ya uso wa nchi. Na kama mwezi ule utawahi kusogea, ungefanya jambo lile lile tena. Mwezi unapotikisika kidogo ukisogea mbali na dunia, husababisha maji kujaa baharini. Unaposhuka, kunafuata kupwa baharini. Ni jeshi kuu la Mungu. Na nilipofikiri kuhusu ile ... hilo likiwa jeshi kuu la Mungu hapo.

34 Sasa, tulienda kulala. Na basi nikaanza kuwazia kwamba hata moja ya hizo haiondoki mahali pake. Zote ziko mahali pake. Na kama kuna msogeo, mahali po pote kati yazo, ni kwa sababu fulani na itakuwa na kutaathiri dunia hii. Nasi tumeona matokeo yake sasa, kutokana na baadhi yazo kusogea kwenye sehemu zao zingine. Husababisha mambo. Inaathiri kila kitu.

35 Nami nikawaza, basi, kama hilo jeshi kubwa kama hilo la mbinguni, linapaswa kushikilia mahali pake, kufanya kila kitu kiwe katika utaratibu, je! vipi kuhusu mchafuko wa jeshi la duniani? Jinsi ambavyo wakati mmoja anatoka kwenye utaratibu, jinsi inavyovuruga kila kitu. Mpango mzima wa Mungu unavurugika wakati mshiriki mmoja anapotoka nje ya utaratibu. Inatupasa kuendelea kujitahidi kudumisha utaratibu wa Roho.

36 Nami ningemwomba Mungu, asubuhi hii, kwamba tungelifikisha hili kwenye ibada halisi ya kuponya, kwamba tungeweza kushikilia sehemu hii ... kundi ambalo tumekusanyika chini ya dari asubuhi hii, katika upatano sana, hata Roho Mtakatifu angemweka kila mshirika wa ule mwili, aliye hapa asubuhi hii, katika upatano sana, hata kungekuwa na kuponya kunakobubujika kwenyewe kwa nafsi na miili, kama tu tungeshikilia mahali petu.

37 Sasa, kama nilivyosema mwanzoni, bibi huyu aliyekuwa na kansa ambayo Daktari Holbrook angechukua ... alikuwa anaenda kuiondoa. Sasa, yule Mungu ambaye alisababisha ile sauti ya kupigapiga mbawa isikike katika ile hospitali, na kuondoa kansa ile bila hata ya kuacha kovu, hamjui kwamba Mungu huyo huyo yupo hapa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na jambo pekee ambalo Yeye anangojea ni kwa je—jeshi Lake kushika mahali pake, kama nyota—kushika mahali pake.

38 Sasa, mnajua, tumekuwa na vita baada ya vita, na matetesi ya vita? Na kama dunia ikidumu zaidi, tutakuwa na vita vingi zaidi. Lakini mnatambua kwamba hasa kuna mamlaka mbili tu katika ulimwengu

wote? Katika ugomvi wetu wote baina ya mataifa, na ugomvi kati ya mmoja na mwingine, na kila kitu, yote yanaingia jumla katika mamlaka mbili. Kuna mamlaka mbili tu, na kuna falme mbili tu; mamlaka mbili, na falme mbili. Mengine yote, mambo madogo madogo, yameunganishwa na mojawapo ya hizo mamlaka. Na mamlaka hizo ni mamlaka za Mungu na mamlaka za Shetani. Hivyo ndivyo ... Kila vita, kila machafuko, kila kitu kinachokuja, aidha kinatawaliwa na nguvu za Mungu ama nguvu za Shetani, maana hizo ndizo mamlaka mbili pekee zilizopo. Na hizo ni mamlaka ya uzima na mamlaka ya mauti. Sasa, hizo ndizo mamlaka mbili pekee.

39 Na Shetani anaweza tu ... Nguvu zake, anazo, ni nguvu zilizopotoshwa za Mungu. Si nguvu halisi. Ni upotovu wa nguvu za Mungu, kila kitu alichu nacho Shetani. Mauti ni uhai uliopotoshwa tu. Uongo ni ukweli uliopotoshwa tu. Mnaona? Uzinzi ni te—tendo lililotumiwa vibaya, tendo la haki likitumiwa vibaya. Mnaona? Kila kitu alichu nacho Shetani ni kitu kilichopotoshwa, bali ni nguvu.

Nasi tupo leo tunaketi hapa, na moja au nyingine ya mamlaka hizo itatutawala sisi. Kwa hiyo hebu na tumfukuze yule mwovu. Hebu na tuchukue mahali petu kama nyota za mbinguni.

40 Kama Biblia inavyosema, "Nyota zipoteazo," katika Kitabu cha Yuda, "zikitoa aibu zao zenyewe kama povu." Nasi hatutaki kuwa nyota zipoteazo; sijui kama *hili* ni kweli, sijui kama *hilo* ni kweli, sijui kama litatukia, sijui ingewezekanaje. Usitangetange. Kaeni kama nyota hizo za mbinguni, kama askari halisi kwenye wajibu wake. Simama pale, ukiamini! Uzima na mauti.

41 Sasa, jeshi, wakati kweli ni jeshi, taifa linajitayarisha kwenda kupigana na taifa lingine, linapaswa kwanza likae chini na kupima kilicho sahihi na kisicho sahihi, na iwapo wanaweza kupigana dhidi ya taifa jingine au la. Yesu alifundisha jambo hilo. Na kama watu wangepigana hivyo, kama mataifa yange—yangeketi chini, na kutulia na kuwazia mambo hayo, pande zote mbili, tusingekuwa na vita tena.

Sasa, tunaona, kama mtu asifanye hayo, kama wakuu wa jeshi la taifa hawaketi chini, kwanza, na kufikiria na kuona ya kwamba wako sahihi, na nia na makusudi yao ni sawa, na kama wana nguvu za kutosha na uwezo wa kushinda jeshi jingine, basi hakika watashindwa.

42 Hapo ndipo Jenerali Custer alipofanya kosa lake baya sana. Jenerali Custer, kama ninavyofahamu, alikuwa na maagizo kutoka serikalini, ya kutokwenda katika nchi ya Sioux, kwa sababu ulikuwa ni wakati wa kidini kwao. Ulikuwa ni wakati wa ibada. Walikuwa wakifanya karamu. Lakini Custer alilewa, naye alifikiri angefanya tu jambo hilo hata hivyo. Yeye angevuka, kama ilikuwa ni amri ama si amri. Na ndipo kwa kweli waliwapiga risasi watu wasio na hatia, wakawatupia risasi. Nafikiri waliwapiga baadhi yao. Ilikuwa ni maskauti, huko nje, wakitafuta chakula, kuwalisha watu wao—wao walipokuwa katika ibada. Naye Custer, alipokuwa anavuka aliwaona akafikiri walikuwa wanawawinda, na kwa hiyo waliwatupia risasi hawa maskauti. Na hawa maskauti wakatoroka, wakarudi. Walifanya nini? Wakatwaa silaha, hawa hapa wanakuja. Na huo ulikuwa ndio mwisho wa Jenerali Custer, kwa sababu hakuketi chini na kuwazia, kwanza.

Hakuwa na shughuli yo yote kule. Hakuwa na haki ya kuwa pale. Alikuwa amewasukumia Wahindi kote kote toka Pwani ya Mashariki, kufikia upande wa magharibi, kwa vyote vyote. Nao walikuwa na mapatano, bali yeye alivunja mapatano hayo. Na wakati alipovunja ule mkataba, ndipo akashindwa vita.

43 Na kwa hiyo jeshi, kwanza, katika kujiandaa kwa vita, kwanza hapana budi kuwe na kuchaguliwa, baadhi ya askari. Yawapasa wavalie kwa ajili ya mapigano. Hawana budi kufundishwa kupigana.

Nami ninaamini ya kwamba vita vikubwa sana vilivyowahi kupiganwa, sasa viko tayari kuanza kazi. Ninaamini ya kwamba Mungu amekuwa akiwachagua askari Wake. Ninaamini amekuwa akiavalisha, akiwafunza. Na mstari wa mbele wa vita sasa umeisha pangwa, tayari kuanza.

44 Vita vikuu, vya kwanza vilivyowahi kupigwa, vilianza Mbinguni, wakati Mikaeli na Malaika zake walipopigana dhidi ya Lusifa na malaika zake. Vilianza kwanza, vita vya kwanza vilikuwa Mbinguni, Kwa hiyo, dhambi haikuanzia duniani, ilianza Mbinguni.

Na halafu ikatupwa chini toka Mbinguni, ikatupwa toka Mbinguni, hadi duniani, na kuanguka juu ya wanadamu. Ndipo vita, kutoka kwa malaika, vikawa vita vya kibinadamu. Naye Shetani akaja kuangamiza uumbaji wa Mungu, kile Mungu alichokiumba kuwa kwa ajili Yake Mwenyewe. Alikuwa, Shetani, amekuwa kukiharibu. Hilo ndilo lililokuwa kusudi lake, ni kuangamiza. Ndipo vita vitaanza hapa duniani, na kuanza ndani yetu, na vimekuwa vikiendelea tangu wakati huo.

45 Naam, kabla ya vita vyo vyote kupangwa, yabidi kwanza wachague mahali pa kukabiliana, au mahali ambapo vita vitapiganiwa, mahali palipochaguliwa.

Katika Vita Vikuu vya Kwanza vya dunia, vilipangwa vizuri sana, katika ardhi isiyo ya mtu na mahali ambapo wangepigania, Na yabidi pawepo na mahali palipochaguliwa.

Kama vile wakati Israeli walipopigana vita na Wafilisti, kulikuweco na—na—na kilima kila upande

walikokusanyika. Na hapo ndipo Goliathi alipotoka na kuyaita majeshi ya Israeli. Hapo ndipo Daudi alipokutana naye, bondeni, wakati alipopita kwenye kijito kidogo kilichopita katikati ya vilima viwili, aliokota mawe.

46 Hapana budi pawe na mahali palipochaguliwa. Na katika hili, kuna ma—mahali palipokubalika na pande zote, ardhi isiyo ya mtu, nao wanapigana mahali *hapa*. Wao hawafanyi hivyo, hawapigani vita moja *hapa*, na moja chini *hapa*, na mmoja hukimbia *huku*. Kuna uwanja wa vita ambapo wanakutana na kujaribu nguvu zao, ambapo kila jeshi hujaribu nguvu zake dhidi ya jeshi lingine, mahali pa kukutania. Sasa, (msipate) kukosa hili.

Wakati vita hivi vikubwa vilipoanza duniani, ilibidi kuwe na mahali pa kukutania. Ilibidi pawepo mahali palipochaguliwa pa kuanzia vita, na kwa vita kuwaka moto. Na sehemu hizo za vita zinaanzia katika nia ya mwanadamu. Hapo ndipo vita vinapoanza. Akili ya binadamu ilichaguliwa kuwa uwanja wa vita, ambapo vilipaswa kuanzia, na hiyo ni kwa sababu kwamba maamuzi hufanywa kwenye akili, kichwani. Sasa, kamwe hawakuanzisha jambo hilo kutoka kwenye madhehebu fulani. Kamwe hawakuanzisha jambo hilo kutokana na jambo fulani la kimitambo. Uwanja wa mapambano haukuanza hapo kamwe. Kwa hiyo, madhehebu hayo hayawezi kamwe, hayawezi kamwe kufanya kazi ya Mungu, kwa sababu mahali pa mapambano, ambapo inakubidi kukabiliana na adui wako, ni katika akili. Huna budi kufanya chaguo lako. Vinakukabili.

Ninataka msichana huyu mdogo hapa, ambaye ni mgonjwa sana, ahakikishe sasa anasikiliza hili, kwa makini sana.

47 Maamuzi hufanywa akilini, kichwani. Hapo ndipo Shetani anakabiliana nawe, na maamuzi hutolewa, kwa sababu Mungu alimfanya mtu jinsi hiyo.

48 Sasa, nina (kama ulikuwa ukiangalia kwenye muhtasari wangu hapa) ramani ndogo iliyochorwa. Nilikuwa nayo hapa si muda mrefu uliopita, kwenye ... iliyotumiwa kwenye ubao. Mwanadamu ameumbwa tu kama punje ya ngano. Ni mbegu. Na mwanadamu ni mbegu. Kimwili, wewe ni uzao wa baba yako na mama yako; na uhai unatoka kwa baba, nyama ya mwili hutoka kwa mama. Kwa hiyo, hizo mbili, pamoja, yai na ile—ile damu, zinakutana. Na katika chembechembe ya damu kuna uhai. Ma mle ndani huanza, kukua kumfanyiza yule—yule mtoto. Sasa, mbegu yo yote ina ganda upande wa nje; upande wa ndani ni nyama, na ndani ya nyama ni chembe ya uhai. Vema, hivyo ndivyo tulivyoumbwa. Sisi ni mwili, nafsi, na roho. Sehemu ya nje ya mwili, ganda; ndani ya huo, dhamira na kadhalika, ni nafsi; na ndani ya nafsi, ni roho. Na roho inatawala mengine yote.

49 Sasa, kama utaketi chini utakapofika nyumbani, na kuchora duara tatu ndogo. Utaona kwamba mwili wa nje una hisi tano ambazo huwasiliana kwazo, na hizo ni kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia. Hizo ndizo hisi tano zinazoongoza mwili wa binadamu.

Ndani ya mwili ni nafsi, na hiyo nafsi inaongozwa na mawazo, dhamira, kumbukumbu, hoja, na upendo. Hicho ndicho kitu ambacho huongoza nafsi.

Lakini, roho, ina hisi moja tu. Roho ... Loo, hebu na tulipate. Roho ina hisi moja, na hisi hiyo aidha inaongozwa, na imani au shaka. Hiyo ni kweli kabisa. Na kuna njia moja tu kwake, hiyo ni uhuru wa kuchagua. Unaweza kukubali shaka au unaweza kukubali imani, mojawapo unayotaka kufanya kazi nayo. Kwa hiyo, Shetani alianzia sehemu hiyo muhimu, kusababisha roho ya binadamu kushuku Neno la Mungu. Mungu alianzia sehemu hiyo muhimu kuweka Neno Lake katika roho ile. Haya basi. Hilo ndilo linalofanya jambo hilo.

50 Kama kanisa hili, sasa hivi lingeweza kuwekwa pamoja, na kuunganishwa pamoja kwa kitu kama hicho ili kwamba kila mtu awe katika moyo mmoja, bila ya shaka hata kidogo po pote, pasingekuwa na mtu mnyonge miongoni mwetu, katika dakika zingine tano. Kusingekuwa na mtu ye yote hapa anayehitaji Roho Mtakatifu ila ambaye angempokea Huyo, kama mngeweza tu kutengeneza hilo jambo fulani. Sasa, hapo ndipo vita huanza, moja kwa moja mawazoni mwako, kama ukitaka.

51 Sasa kumbukeni, si Sayansi ya Kikristo, sasa, akili juu ya maumbile ya asili. Hilo halina ... Akili hupokea Uzima, ambao ni Neno La Mungu, na hapo huleta Uzima. Wazo lako tu halifanyi hivyo. Lakini, Neno la Mungu, likiletwa katika mkondo wa wazo lako. Mnaona? Siyo wazo, kama Sayansi ya Kikristo inavyolifanya, akili juu ya maumbile ya asili. La. Hilo silo.

Lakini, akili yako inakubali jambo Hilo. Hulishikilia. Akili yako huongozwa na nini? Roho yako. Na roho yako hulinasa Neno la Mungu, na hicho ndicho kitu kilicho na Uzima ndani Yake. Linaleta Uzima ndani yako. Loo, ndugu! Hilo linapotendeka, wakati Uzima hushuka chini kwenye mkondo ule, kuingia ndani yako, Neno la Mungu linadhihirishwa ndani yako. "Ninyi mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

52 Basi hilo linafanya nini? Toka katikati ya moyo, ambayo ni nafsi, tokea hapo huenda, kulisha kila mkondo. Shida yake ni kwamba, tunasimama humu ndani tukiwa na shaka nyingi, tukijaribu kukubali

yaliyo *huko* nje. Huna budi kukomesha jambo hilo; na kushuka kwenye mkondo ule na Neno la kweli la Mungu, na ndipo linatoka, lenyewe, bila ya kushurutishwa. Ni kile kilicho ndani. Hicho ndicho kitu cha maana, ni kile cha ndani. Shetani huanza kutukabili kutokea ndani.

53 Sasa, unasema, "Mimi siibi. Sinywi pombe. Sifanyi mambo haya." Hilo halina uhusiano wowote nalo.

Mnaona, ni mle ndani. Haidhuru wewe ni mzuri iliyoje, ni uadilifu iliyoje, ni mkweli iliyoje, mambo hayo yanaheshimiwa. Lakini Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili." Mnaona? Hapana budi kuwe na jambo fulani linalotukia ndani. La sivyo, hayo ni mambo ya kuigiza, kwani chini ndani ya moyo wako unatamani kutenda jambo hilo kwa vyo vyote. Hakiwezi kuwa cha bandia. Hakina budi kuwa cha halisi.

54 Na kuna njia moja tu ambayo hicho chaweza kushukia, na hiyo ni kwa njia ya uhuru wa kuchagua, huja katika nafsi, kwa mawazo yako. "Kama vile mtu afikirivyo moyoni mwake, ndivyo alivyo." Kama ukivambia mlima huu, 'Ng'oka' na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba ulilosema litatukia; litakuwa lako." Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Haya basi. Mnaona? Huo ndio uwanja wa vita. Kama ungeanza tu hilo, kwanza.

55 Tuna shauku sana kuona mambo yakitendeka. Tuna shauku sana ya kumfanyia Mungu jambo fulani. Maskini bibi huyu si ... anamtamani sana, bila shaka anatamani kuishi Anataka kuwa mzima. Wengine wako hapa, wanataka kupona. Na tunaposikia kuhusu jambo hilo, kama yule daktari, kufufuliwa kwa wafu, mambo makuu ya uweza ambayo Mungu wetu ametenda, basi tunatamani mno. Na jambo ni kwamba, tunajaribu kwa hisi hizi, kushika jambo fulani hapa, kama dhamiri.

56 Watu wengi, sana mara nyingi, wamekosa kuelewa vema Neno. Nami nimeeleweka vibaya na jambo hili, kwa kufanya miito ya madhabahuni. Nilisema "sishikili sana miito ya madhabahuni," simaanishi kwamba hupaswi kutoa mwito wa madhabahuni.

Bali mtu fulani anamshika mtu mkono akasema, "Loo, Ndugu Yohana, unajua nini? Mimi na wewe tumekuwa majirani wakati huu wote. njoo huku madhabahuni, piga magoti." Yeye anafanya nini? Laiti ningalikuwa na ubao hapa, ningeweza kuwaonesha yale anayofanya. Anajaribu kutenda kazi kwa nafsi yake, katika upendo. Hilo halifai kitu. Hiyo siyo ile njia. Hakika, siyo.

Labda yeye anafanya kazi katika (nini?) Kumbukumbu, kupitia hisi ya nafsi yake. "Loo, Ndugu John, ulikuwa na mama mzuri sana. Alikufa muda mrefu uliopita." Kumbukumbu! Mnaona? Huwezi kufanya hivyo.

Halina budi kuja kwa njia ya uhuru wa kuchagua. Wewe, mwenyewe, ruhusu Neno la Mungu... Huji kwa sababu mama yako alikuwa mwanamke mzuri. Huji kwa sababu wewe ni jirani mwema. Unakuja kwa sababu Mungu anakuita uje, nawe unamkubali juu ya msingi wa Neno Lake. Neno hilo ndilo linalomaanisha kila kitu. Hilo Neno! Kama unaweza kuondoa kila kitu njiani, dhamiri yote, hisi zote, na uache tu Neno liingie, Neno hilo litazaa kabisa.

57 Hapa, mnaona limefunikwa na kitu gani? Unasema, "Vema, sasa," unasema, "vema, hizi, dhamiri na hisi, na kadhalika, hazina uhusiano wowote nalo, Ndugu Branham?" Hakika zinahusika! Lakini iwapo utaliruhusu Neno liingie na kulifunika na dhamiri, basi haliwezi kukua, litakuwa neno lemavu.

Je! uliwahi kuona punje nzuri ya mahindi iliyopandwa ardhini, na kuachia kijiti kiiangukie? Itakua imepinda. Mzabibu wowote, chochote ambacho hukua kitafanya hivyo, kwa sababu kitu fulani kimekizuia.

58 Vema, hiyo ndiyo shida ya Imani yetu ya kipentekoste leo. Tumeacha mambo mengi sana yaizuie, Imani ambayo tumefundishwa, Roho Mtakatifu ambaye amekuwa akiishi ndani yetu. Tumeachilia mambo mengi sana, tukimwangalia mtu mwingine.

Na ibilisi sikuzote anajaribu kukuonesha kushindwa kwa mtu, lakini anajaribu kukuondoa kwenye ushuhuda halisi ambao ni wa kweli. Yeye atakuelekeza kwa mnafiki, wakati fulani, ambaye alitoka akaenda kuiga kitu fulani. Yeye hakufanikiwa, kwa sababu alikuwa anaigiza. Lakini kama linatoka kwenye chanzo halisi cha Neno la Mungu, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu haliwezi kupita," halina budi kukaa pale.

Unaelewa hilo, dada?

59 Halina budi lipokewe akilini; kisha linaaminiwa kwa moyo. Ndipo Neno la Mungu linakuwa jambo halisi; ndipo kila hisi za nafsi na mwili zinasuguliwa sana kwa Roho Mtakatifu. Ndipo wewe ni hisi ya Mungu; wewe ni dhamiri ya Mungu; kila kitu kinachomcha Mungu kinatiririka kupitia kwako. Hakuna shaka mahali po pote. Hakuna kitu kinachoweza kujiinua.

Hakuna cho chote kinachoweza kuja kwenye kumbukumbu na kusema, "Vema, ninakumbuka Binti Jones alijaribu kumtumaini Mungu na Bibi Fulani. Bibi Doe alijaribu kumtumaini Mungu kwa ajili ya uponyaji, wakati mmoja, naye akashindwa." Mnaona?

Lakini kama mkondo ule umefagiliwa na kutakaswa, na kujazwa ndani kwa Roho Mtakatifu, hilo hata



halikumbukwi, haidhuru kuhusu Bi Jones na yale aliyofanya. Ni wewe na Mungu, pamoja, na si mtu mwingine ila ninyi wawili. Haya basi. Hivyo hapo vita vyako. Muue papo hapo mwanzoni. Mkomeshe kabisa anapokuja. Si unaweza kuendeleza vita muda gani. Ni kuvikomesha sasa hivi!

60 Kama utakuja, na utashikilia hizo kumbukumbu, na dhamiri, na kila kitu kufikiria kuhusu, "Naam, huenda nikashindwa. Huenda ikawa si sahihi." Usifanye hivyo, hata kidogo.

Tupilia kando kila kitu na ufungue ule mkondo useme, "Mungu, Neno Lako ni Kweli Milele, Nalo ni kwa ajili yangu. Kama kanisa lote likishindwa, kama ulimwengu mzima ukishindwa, hata hivyo siwezi kushindwa, kwa sababu ninachukua Neno Lako." Hivyo hapo vita. Jambo ndilo hilo .

61 Kwa nini Mwenyezi Mungu aondoe kansa kwenye titi la mwanamke, bila kovu, na kumwacha mtoto alale na afe? La, bwana.

62 Msichana mdogo alikuja hapa, si muda mrefu uliopita, kutoka shule ya sekondari. Mama yake akanipigia simu, akasema, "Ndugu Branham, msichana wangu ana ugonjwa wa kuvimba wengu na ini." Hiyo ni kansa, huwa inafanya marungurungu. Nao madaktari wakachukua kipande kilichotoka kilichotoka kwenye koo lake, wakakipeleka, na kilikuwa ni ugonjwa wa kuvimba wengu na ini kweli.

Kwa hiyo akasema, "Kngine kikitumbukia huenda kikatumbukia katika moyo wake. Hilo likitukia, ataaga dunia." Kasema, "Yeye hana ... Akasema, "yeye ana, namna vinavyomeguka, popote, ataishi tuseme, yapata miezi mitatu."

Yule mama akasema, "Nifanye nini? Nimrudishe shuleni?"

Kasema, "Mwache aende kwa sababu labda atakufa ghafla." Kisha akasema, "Mwache tu aende akaishi maisha ya kawaida, awezavyo. Usimwambie kitu kuhusu hilo jambo."

Kwa hiyo yule mama akaniambia, "Nifanye nini?"

Nikasema, "Mlete hapa na umweke kwenye mstari wa maombi." Nami nikasema, "Njoo pamoja naye." Nikahisi jambo dogo geni.

63 Na wakati yule msichana alipokuja asubuhi ile, na midomo ya samawati, kutokana na kujipodoa, na shule hiyo inayo mambo hayo. Na—na maskini msichana huyo akaja kule. Sikujua yeye ni nani; ilikuwa wanipigie simu. Nikamshika mkono. Nikasema, "Habari za asubuhi, dada." Huyo hapo. Huyo alikuwa ndiye. Mnamo muda kidogo nalitazama kule chini kwa mamaye na kuona wote wawili bila Mungu, bila Kristo. Nikasema, "Unawezaje kutarajia uponyaji kwenye misingi hii? Utamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako binafsi?" Nikasema, "Je! Utakuja kwenye kidimbwi hiki hapa na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako?"

Wakasema, "Tutafanya hivyo."

Loo, mnajua kilichotukia. Huenda mwanamke huyo ameketi hapa asubuhi ya leo. Wengi wenu mnajua kisa hicho. Ndugu Mike Egan, mmoja wa wadhamini hapa, alifuatilia kisa hicho. Hiyo imekuwa kama miaka minne ama mitano iliyopita. Msichana huyo mchanga mdogo alirudishwa kwa daktari, hakuna hata alama ya ugonjwa wa kuvimba wengu na ini ulioonekana ndani yake.

64 Sida ilikuwa ni nini? Ilikubidi kufungua ule mkondo, kwanza. Huna budi kumchukua Askari, Roho Mtakatifu, kuwekwa mahali pa vita, ambaye huchukua Neno la Mungu. Yeye ni Neno. Naye anasimama pale, hakuna kitu kitakachomzuia wakati huo. Hakuna kitu cho chote. Kila moja ya hiyo mikondo mingine imefagiliwa. Ni kama tu vile chombo cha mtambo mkuu cha kuchemshia maji chenye bomba lililozibwa; unaweka moto ndandi;, nalo litalipua chombo chako. Hiyo ndiyo shida ya Wakristo wengi sana waliolipuliwa, ni kwa sababu hawaisafishi mikondo, hawashuki wakaingia mle ndani. Inakubidi kuisafisha, dhamiri, kumbukumbu, fikara, kuweka kando kila kitu, na kuja kutoka ndani hadi nje, pamoja na Neno la Mungu lisiloghoshiwa, kwamba Hilo ni Ukweli.

Haidhuru kama elfu kumi walikufa upande *huu*, leo, wakitumaini; elfu kumi walikufa upande *huo*, kesho, wakitumaini; hilo halina uhusiano wo wote nami. Mimi ni mtu binafsi. Mimi ndiye ninayetumaini. Mimi ndiye ninayeamini jambo hilo. Nasi tunaona nyuma huko, kama tukitaka kufungua mikondo yetu basi, kama tunaweza, na kuona. Tunamwona *huyu* na *yule*, na *huyu* na *yule*, maelfu yao, wakashuhudia.

65 Lakini ibilisi atajaribu kurudi moja kwa moja tena. Mnaona, kama anaweza kuingia mle, hata kidogo, amelishinda jeshi lako papo hapo.

Kama una hisi zako, mnaona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia, ni sawa, bali usizitumie isipokuwa zikubaliane na Neno. Ziko sawa, bali kama hazipatani na Neno, usizisikilize. Sasa, mawazo, dhamiri, kumbukumbu, fikara, na upendo, ziko sawa, kama zikiambatana na Neno. Bali iwapo upendo wako haupatani na Neno, ukatae. Utalipua bomba upesi sana. Mnaona? Kama hoja yako haikubaliani na Neno, iache. Hiyo ni kweli. Ule mtambo ... Kama kumbukumbu zako, kama mawazo yako, kama dhamiri zako, cho

chote kile hakiambatani na hilo, kile kilicho ndani, kiondoe!

66 Una nini basi? Una mfumo wa jua. Haleluya! Ni, Mungu aliziweka nyota katika utaratibu kisha akasema, "Ning'inieni hapo hata nitakapowaita." Zinakaa pale. Hakuna kitu kitakachozisogeza. Wakati Mungu anapoweza kumpata mtu mikononi Mwake, hata yeye aweze kusafishwa hisi, dhamiri na kila kitu, mpaka inasimama na Mungu nyuma yake, katika Roho, hakuna pepo duniani awezaye kuingiza shaka mle ndani. Hiyo ni kweli.

Yeye anakuja na kusema, "Hujisikii vizuri zaidi."

67 Dhamiri yako hata imekufa, kwa jambo hilo. Bomba ni safi sana hata linapaza sauti, "Haleluya!" Tundu hilo linapiga filimbi; "Mungu atukuzwe!" Linatoa sauti, kwa hakika, ni safi na dhahiri sana, kwa Neno la Mungu kutenda kazi kwake, Uweza wa Mungu. Mnaona? Hilo ndilo jambo muhimu.

68 Hapo ndipo penye uwanja wako wa vita. Uwanja wako wa vita uko nyuma hapa mwanzoni, nyuma hapa kwenye nafsi, nyuma kwenye akili yako inayofunguka. A—akili ndiyo lango la kuingilia kwenye nafsi, namaanisha lango la kuingilia kwenye roho. Akili yako hufunguka na kumkubali Roho, au inamkataa Roho. Unaweza kuwa na dhamiri ndogondogo, na hisia ndogondogo, na mishtuko midogomidogo, mambo yote haya. Hilo halina uhusiano wowote na hilo. Hiyo ni mihemuko midogo tu na kadhalika. Lakini ijapo kwenye jambo halisi, akili yako hufunguka. Akili yako aidha inalikubali au inalikataa! Ndivyo ilivyo, marafiki.

Mungu, jalia asiweko mtu ye yote kati yao atakayelikosa.

Mnaona, ni akili yako ambayo hufungua mlango; ama kufunga mlango, na kusikiliza dhamiri zako, kusikiliza kumbukumbu zako, kusikiliza upendo wako. Bali wakati akili yako inapojifungua yenyewe kwa mambo haya, na kumruhusu Mungu, Roho wa Neno Lake, aingie, Huyo hutimua kila upuzi nje! Kila shaka imetoweka. Kila hofu imekwisha. Kila mhemko wa shaka umekwisha. Kila hisia imekwisha. Hakuna kitu kinachosimama pale ila Neno la Mungu, na Shetani hawezi kupigana na Hilo. La, bwana. Hawezi kupigana Nalo. Sasa, tunajua hiyo ni kweli.

69 Vita hivi vimepiganwa tangu siku ya bustani ya Edeni, vita katika akili ya binadamu. Shetani aliianzisha. Alifanya nini alipokutana na Hawa? Yeye hakulikana Neno la Mungu, bali alilipaka chokaa. Aliziba baadhi ya mikondo midogo hapa mahali fulani. Akasema, "Lakini hakika Mungu ..." Mwanzo 3:1. Mnaona? "Hakika, Mungu, mambo haya yote ambayo Yeye—Yeye—Yeye aliahidi ..." Yeye alijua Neno lilikuwa ni kweli. Lakini alijua hangeweza kuja tu moja kwa moja na kulilipua Hilo, kwa kishindo jinsi hiyo, bali yeye—yeye—alilifunika kwa sukari.

70 Kama mama alivyozoea kutunyweshwa dawa, naye angejaribu kuweka maji ya machungwa katika mafuta ya mbarika. Jamani, afadhali kunywa mafuta ya mbarika bila ya maji ya machungwa! Kitu cho chote ambacho ni cha kinafiki! Mnaona? Yeye ... Tuzoea kulazimika kuamka wakati wa usiku, naye angetupa mafuta ya samaki, kwa ajili ya ugonjwa wa kusongwa na koo. Naye angeweza mafuta ya samaki, na kuyatia sukari; unaona, kinafiki kwa namna fulani. Lakini yangeviwasha tu vivimbe vyako vya kooni, yakiwa yanashuka, baada ya ile sukari kwisha.

71 Vema, hivyo ndivyo ilivyo, rafiki. Shetani hujaribu ku—kuwa mnaofiki juu ya jambo hilo. Yeye anajaribu kukuonesha kitu bora zaidi, njia rahisi, mpango wa busara zaidi. Lakini hakuna mpango wa busara zaidi ya ule Mungu aliouweka hapo mwanzo, Neno Lake. Shikilia hilo Neno. Lishike Hilo kabisa! Liache Hilo likushike kabisa. Dumu pale pamoja Nalo. Hivyo ndi—hivyo ndivyo ilivyo.

72 Vita viliwaka moto wakati Hawa alipofungua akili yake kusikiliza hoja zake. Hilo ndilo bomba ililoingilia. Huo ndio ule—ule mkondo ilimotirikikia, hoja zake. Yeye, katika nafsi yake, alihoji.

Macho yake yalikuwa ni kuona. Alimwona yule nyoka. Yeye alikuwa mrembo, mzuri wa uso, mzuri sana kuliko mumewe. Alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwituni, naye alikuwa labda mwanamume mzuri zaidi kuliko mumewe; Alionekana kama mnyama mkubwa wa kiume aliyesimama pale. Jinsi alivyokuwa mkubwa! Naye alikuwa anajaribu kumwambia mwanamke jinsi kilivyokuwa kitu kizuri.

Na jambo la kwanza mwanamke alilotenda, alifungua bakili yake. Naye alipolifungua, hoja za kibinadamu zililikamata. "Kwa nini, hivi jambo hilo lisingalikuwa jambo la kuisimua!"

73 Hilo ndilo jambo atendalo kwa mwanamke leo. Mwanamke fulani mwenye mwanamume mdogo anayependeza, anapata jitu kubwa, pandikizi la mwanaume. Mwanamume huyu atajaribu kuanzisha mahojiano. Kumbuka, huyo ni Shetani. Huyu ni Ibilisi. Ama, vinginevyo, mwanamume kwa mwanamke, mwanamke kwa mwanamume, kwa vyo vyote vile. Yeye anafanya nini? Anatenda kazi katika ule ustadi wa kuhojiana, ile dhamiri au jambo fulani, huanza kuingia ndani.

74 Bali lipe Neno la Mungu nafasi ya kwanza. Mtu hawezi hata kuja ... Hawezi kutenda dhambi ... Haleluya! Hili hapa. Hili linakuja, jipya. Mtu hawezi kutenda dhambi mpaka kwanza atupilie mbali Neno la Mungu. Hata hawezi kutenda dhambi, hiyo ni, kutokuamini. Mpaka kwanza atakapoliandoa Neno la

Mungu, Uwepo wa Mungu, hawezi kutenda dhambi.

Hawa asingeweza kutenda dhambi mpaka alipoweka kando Neno la Mungu, akafungulia mkondo wake wa mahojiano katika nafsi yake, naye akaanza kutoa hoja. “Mbona, hakika. Mume wangu hajawahi kuniambia mambo haya, lakini ninaamini ya kwamba wewe ... Yeye aliniambia sipaswi kufanya jambo hili, lakini, unajua, unalifanya halisi sana na dhahiri sana. Ni—ninaamini lingekuwa jambo zuri sana, kwa sababu unalifanya dhahiri mno kwangu.” Mnaona, hivyo hapo vita vya kwanza. Na kwa vita vile, amesababisha kila vita vingine. Na kumwagika damu kwo kwote kulikowahi kuja kulisababishwa pale pale katika Edeni. Yeye hakuliamini Neno la Mungu.

75 Na kama yodi moja ndogo ya Neno la Mungu haikuaminiwa, ilisababisha taabu zote hizi, tutarudije, huku hatuliamini Neno? Huwezi kufanya hivyo. Yakubidi ufungie nje mambo haya mengine yote, dhamiri, kumbukumbu na tuseme ... hoja na haya mambo mengine yote, “Tukitupilia mbali mahojiano.” Hatuhoji juu ya jambo hilo, hata kidogo, hakuna hata kidogo.

Tunalikubali tu Neno juu ya msingi, “Mungu alisema hivyo”; na linafanya kijito kati yako na Mungu. Kila mkondo unafunguka kati yako wewe na Mungu, basi.

76 Hivyo hapo vita, mstari wa mbele, hasa. Hebu na tusitumie bunduki aina ya ishirini na mbili; hebu tuchukue bomu la atomiki. Hebu na tufanye kazi hiyo vizuri. Hebu na tupate bomu la atomiki la Mungu. “Ni kitu gani, Ndugu Branham?” I-m-a-n-i katika Neno Lake. Hilo ni bomu la atomiki la Mungu. Linatimua maradhi na pepo, kulia na kushoto. Hilo—huyaangamiza. Huyabagua ... Loo, ni ... Huyaharibu tu. Nalo huvunjavunja kila kitu ambacho hakimchi Mungu. Wakati hilo bomu la imani linaposhuka mle ndani, likiwa na Neno la Mungu nyuma yake, hutimua kila pepo, kila maradhi, kila ugonjwa.

Unasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham? Basi kwa nini linatenda, kwa watu fulani, na sio kwa wengine?”

77 Ni kwa sababu ya ule mkondo. Unaweza kuangalia nje na ulione hilo. Lakini huna budi kuwa nalo humu ndani, ukiangalia upande *huu*. Siyo nje huko, ukitazama ndani; yakubidi uwe ndani, ukiangalia nje. Mnaona? Huwezi kupitia kwa hoja. Huwezi kupitia mambo haya mengine. Huna budi kushuka moja kwa moja kwenye mkondo wa Mungu, moja kwa moja kwenye nafsi. Na unafanyaje jambo hilo? Mkondo wa mwisho ni upi?

Ita ninii ... moja kwa moja chini. Unasema, unalihisi, “Loo, na—naweza kulihisi. Naam, hilo hapo. A-ha. Loo ni—ninaweza kunusa harufu yake, au na kadhalika. Mambo haya yako pale. Naam.” Jambo jingine, unajadili, “Vema, yaonekana yampasa kujua ambalo analizungumzia. Daktari anasema siwezi kupona. Hilo linapaswa kuwa hivyo.” Mnaona, papo hapo ume—umekosea. Huyo ni Ibilisi amesimama hapo. Huyo ni Ibilisi akiingiza mambo haya ndani yako. Usiliamini.

“Haleluya! Neno la Mungu lilisema nitaninii ... 'Juu ya mambo yote, ningetaka uwe na afya njema.' Hiyo ni kweli.” Unawezaje kuwa askari halisi huko nje? Unaona, “Ninataka uwe na afya njema.”

78 Hiyo hapo, papo hapo, mikondo hiyo. Unaipata tu, fungua. Usiachilie.

Basi kama Shetani anaweza kupitia pale, aingie kwa dhamiri hizi na mambo haya yote, basi anafikia moja kwa moja chini hapa mwisho wa nafsi, katika akili. Sasa, kama anaweza tu kukupata ... Kamwe huta—kamwe hutaangalia hata moja yao mpaka kwanza umemruhusu aingie *hapa* ndani. Inakubidi kumruhusu aingie. Ndipo anapoingia, ametawala. Basi anafanya nini? Anaanza kutumia dhamiri. Anaanza kutumia *hili*, anaanza kutumia njia *hii*. Ni kitu gani? Kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia, mawazo, dhamira, kumbukumbu, hoja, upendo. Anaanza kutumia mikondo yote hiyo midogo mbalimbali, maadamu angeweza kuingia ndani, juu ya hii hapa. Yeye hana budi kuingia akilini mwako, kwanza, nawe huna budi kukubali jambo hilo. Inaweza ... Sikiliza. Anaweza kukugongagonga, bali haiwezi kukufikia mpaka utakapokubali jambo hilo.

79 Wakati Shetani alipomwendea Hawa, na kusema, “Unajua, tunda hilo ni zuri.” Alisimama kwa muda kidogo. Loo, hapo ndipo alipofanya kosa, wakati aliposimama kwa muda kidogo.

Usisimame bure. Una Ujumbe. Yesu yu hai. Mungu ni Mponyaji. Huo ndio Ujumbe. Usisimame bure, hakuna hoja, wala cho chote kile.

Lakini yeye alisimama kwa muda kidogo. Hapo ndipo Shetani alipoingia moja kwa moja kwenye akili hiyo. Kasema, “Vema, linasikika la busara.” Loo, usifanye hivyo. Hebu chukua tu yale Mungu aliyosema.

80 Ibrahimu, vipi kama angalisimama kwa hoja, wakati Yeye alipomwambia atapata mtoto kwa Sara, na mke wake alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano na yeye sabini na mitano? Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, na Sara alikuwa—naye alikuwa na tisini; yeye, bado, yeye—yeye—yeye alikiri ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa kweli. Naye akaviita vitu hivyo, ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwako. Mnaona? Yeye ... Hata tumaini, kulikuwako na tumaini lolote? Hata hakutumia tumaini.

“Vema,” unasema, “natumaini ninaweza kupata afya. Natumaini nitakuwa mzima. Natumaini nitampata Roho Mtakatifu. Natumaini mimi ni Mkristo. Natumaini nitafanya jambo hili.” Hutaki jambo hilo.

Ibrahimu hata hakuliangalia hilo. Amina. “Kinyume na tumaini, angali aliamini Neno la Mungu.” Imani iko zaidi ya tumaini. Imani hutokea nyuma *huku* upande, wa ndani. Imani inatoka *hapa*.

Anaingiaje ndani? Kupitia akili hii, huu—mlango huu, mstari wa mbele wa vita akisimama pale.

81 Sasa, mpango wa vita unapokamilika! Sasa, Ibilisi ameketi moja kwa moja kwa kila moyo, asubuhi ya leo. Ameketi, katika moyo wa msichana huyu mdogo. Yeye anaketi mioyoni mwenu. Yeye ameketi kila mahali pale. Yeye anasema, “Loo, nimekuona ukijaribu hapo awali. Nimesikia hayo hapo awali.”

Mtupe nje. Hivyo tu. Mtupe nje. Biblia ilisema nini hapa, somo letu? “Kumtupa nje.” Hiyo ni kweli. “Kumtupa nje.” Tumefunzwa.

82 Nadhani, “Hivi sisi wahubiri tuna shida gani?” Sijui tumekuwa na mafunzo ya namna gani.

Mungu anafundisha kwa ajili ya vita hivi vikuu. Mathayo 24 ilisema pale, na pia Danieli 12, ilisema, “Kutakuwako na wakati wa taabu, ambao haujapata kuwako duniani kabla.” Nasi tunaishi katika wakati huo, wakati utamaduni, na elimu, na kadhalika, vimevunja Neno la Mungu, na kuingia katika hoja na kadhalika. Vita vinapiganwa sasa. Ni nani atakayesimama? Haleluya! Vita viko tayari kuanza. Vimeandaliwa sasa. Angalia jinsi tulivyo na upinzani mkuu kule ng'ambo.

83 Ni nani atakayekuwa kama Daudi? Kasema, “Mnasimama na kumwacha Mfilisti huyu asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye Hai! Nitaenda kupigana naye.” Amina. Mungu anataka wanaume na wanawake asubuhi ya leo ambao wanaweza kusimama na kusema, “Nitamchukua Bwana kwa Neno Lake.” Amina. Haidhuru ni kitu gani kinachoshindwa, ambapo *hili* na *lile*, na kile *yule* alichofanya. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Enyi akina Sauli na kadhalika, kama mnamwogopa, rudini nyuma mnapopaswa kuwa. Lakini, jeshi la Mungu linasonga mbele, amina; watu mashujaa, watu wa—wa—wa imani, wenye nguvu, wenye akili. Si lazima wawe werevu. Si lazima waelimishwe. Hawana budi kuwa mikondo. Mungu huchukua mikondo hiyo midogo.

Alisimama kwa muda kidogo, kujadili, akisema, “Vema, sasa, hebu tuone.” Vema, kama tu, vipi kama

...

84 Maskini mwanamke huyu mdogo, asubuhi ya leo, hapana shaka kwamba daktari amemwambia, yuko karibu mwisho wa safari, “Hakuna kitu kingeweza kufanywa.” Vema, sasa, huyo ni daktari huyo. Simlahumu. Mtu huyo ni mtu wa kisayansi. Ameona kwamba ugonjwa umeushinda mwili wa mtoto. Hautibiki. Yeye hana dawa itakayouzuia.

Vivyo hivyo ile saratani ilimshinda mwanamke yule, hakika, kifo kilikuwa kimemshinda mtoto yule, bali Kapteni wetu Mkuu, haleluya, wa jeshi hili kubwa, Yeye ndiye Ufufuo na Uzima. Hakuna kitu kinachoweza kumshinda Yeye. Haleluya!

85 Ubongo wa jeshi uko katika makapteni wake, akili. Rommel, huko Ujerumani, alikuwa ndiye ubongo wa Ujerumani; siyo Hitler, Rommel! Hiyo ni kweli. Eisenhower! Wanajeshi! Patton! Hao watu waliokuwa mstari wa mbele vitani, inategemea walitoa amri kwa njia gani. Wewe mfuate kapteni wako, kama yeye ni jemadari mzuri. Kama yeye ni mtu anayefaa, kama yeye ni jemadari wa nyota nne, kama amehakikishwa, kama amehakikishwa kuwa anafaa, mfuate. Ingawa yaweza kuonekana si sahihi, kwako, songa mbele vitani. Fanya kama alivyokwambia.

86 Haleluya! Tuna Mkuu wa nyota tano, aliyeandikwa J-e-s-u-s, akituwekea nyota tano, i-m-a-n-i. Yeye hajashindwa vita kamwe. Haleluya! Alishinda mauti, kuzimu, na kaburi. Ondoeni pepo njiani. Yeye ndiye yule Kapteni Mkuu. Kwa hiyo, ibilisi hata hayupo kwenye picha.

87 Vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa viko tayari sasa hivi. Hakika, viko tayari. Loo! Haleluya!

Ninapowazia jambo hilo! Niliposimama na kumwalia akifanya mambo, nikimwona akifunua mambo, akifungua mambo, akisema, “Itakuwa *hivi* na *vile*,” ndivyo ilivyo! Loo, angalia nyuma *hapa*, na useme, “Ni nani huyu Kapteni mkuu?” Loo, siangalii nyuma na kuona kama ni Daktari *Fulani*. Ninaona yale Kapteni aliyosema. “Yeye ndiye Kapteni wa wokovu wetu.” Haleluya! Wokovu ni nini? Ukombozi! Utukufu! “Yeye ndiye Kapteni wa wokovu wetu.”

88 Saa muhimu ya kushambulia imewadia. Haleluya! Askari, mwenye silaha zinazong'aa, bendera zinapepea! Imani na mashaka vimejipanga tayari kwa mapambano, katika maskani hii, asubuhi ya leo; shaka upande mmoja, imani upande mwingine. Enyi askari, simameni kwenye sehemu zenu. Haleluya! Nahodha wetu, ile Nyota ya Asubuhi, anaongoza. Yeye kamwe harudi nyuma. Yeye (kamwe) hajui neno kurudi nyuma. Haimbidi kurudi nyuma. Amina. Hakika.

Vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa, vinaendelea papa hapa sasa, naam, bwana, kati ya uhai na

mauti, kati ya magonjwa na afya, kati ya imani na shaka, loo, jamani, kati ya uhuru na utumwa. Vita vinaendelea! Ng'arisheni mikuki yenu, enyi askari. Safisheni silaha. Mungu anawatayarisha askari Wake. Amina. Mungu hupaka mafuta jeshi Lake.

89 Marekani huvalisha askari wao vizuri kadiri wanavyoweza kuwavalisha, kofia za chuma, na dirii, na cho chote walicho nacho, vifaruu vyenye silaha, na cho chote wanachoenda nacho.

Mungu hulivalisha jeshi Lake. Haleluya! Tunatumia vifaa vya aina gani? Roho wa Upanga, Neno la Mungu! Amina! "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili," Waebrania 4, "huchoma hata kugawanya mifupa, hata ma—mafuta ya mifupa, hata huyatambua mawazo ya moyo," Neno la Mungu! Kuamini Neno Lake, na hivyo ndivyo ambavyo Mungu huvalisha silaha.

90 Hilo ndilo Yeye alimpa Hawa ajivike. Naye akavunja silaha yake. Angefanyaje jambo hilo? Kwa kufungua akili yake kuhoji. Huhojiani na Neno la Mungu. Halina hoja. Ninyi ... Ni Neno la Mungu tu. Hakuna —hakuna shaka juu Yake. Hakuna hoja juu Yake. Ni Neno la Mungu. Hilo latosha. Jambo ndilo hilo. Hilo latosha milele.

Unaona ninalomaanisha, mpenzi? [Huyo dada mgonjwa anasema, "Amina." — Mh.] Ni Neno la Mungu. Mungu aliahidi jambo hilo. Mungu alisema hivyo.

91 Wakamwambia Ibrahimu, "Unajuaje utampata mtoto huyo?"

"Mungu alisema hivyo." Hilo lilitosha.

"Vema, mbona hunaye?"

"Sijui nitampata lini, lakini nitampata. Mungu alisema hivyo. Hilo halitanizuia hata kidogo." Yeye aliwaita- ...

"Kwa nini usirudi nyumbani kwenu ulikotoka?"

"Mimi natakiwa kuwa msafiri na mgeni katika nchi hii." Amina! ...?... "Mungu alitoa ahadi. Mungu atanipa mtoto papa hapa kwenye nchi hii ambapo Yeye amenipeleka." Haleluya!

92 Mungu atakuponya moja kwa moja katika mazingira haya ya Roho Mtakatifu, ambapo alikutuma. Mungu atakupa hilo. Liamini tu. Amina. Fungueni hayo mabomba ya nafsi na mwili, hisi na dhamiri, na hebu ruhusu Maneno ya Mungu yapenye kwanza, chukua hiyo akili. Hapo ndipo penye uwanja wa vita.

Siyo useme, "Vema, kama ningeweza kulihisi, kama ningehisi utukufu wa Mungu ukishuka! Loo!" Hilo halina uhusiano wowote nalo; hata kidogo.

Fungua hiyo akili. Huo ndio uwanja wa vita. Hapo ndipo ambapo vita hujipanga, papa hapa kwenye mstari wa mbele, akili yako. Ifungue, na useme, "Mimi ... Kila shaka, ninatilia shaka mashaka yangu." Amina. "Ninatilia shaka mashaka yangu sasa. Ninaamini Neno la Mungu. Mimi hapa ninakuja, Shetani." Kitu fulani kitatukia. Hakika, kitatukia. Naam, bwana.

93 Yeye huwatia mafuta watumishi Wake kwa Roho Wake. Yeye huwapelekea malaika. Watu hucheka jambo hilo wakati mwingine, malaika. Hebu ni—hebu tu nifungue mahali fulani hapa pamoja nanyi, kwa muda kidogo. Hebu tufungue Waebrania hapa, dakika moja. Waebrania sura ya 4, sura ya 4, na hebu ... Ninamaanisha, mlango wa 1 wa Waebrania, na hebu tufungue aya ya 14.

*Je! Hao si roho watumikao, wakitumwa kutoka ... wakitumwa kuwahudumu wale watakaorithi wokovu?*

*... Je! yuko malaika ambaye Yeye alimwambia ... "Uketi mkono Wangu wa kuume ...?"*

*... Malaika wote wa Mungu ...*

94 Sasa, hapa Biblia inarudi moja kwa moja na kutwambia hapa, ya kwamba Mungu huwatuma malaika. Utukufu! Ni nini? "Roho watumikao." Utukufu! Roho wanaotumika, wanatumwa (wapi?) Toka Uweponi mwa Mungu. Kufanya nini? Kuhudumu Neno Lake. Amina! Hupaswi kuhudumu theolojia fulani ya kundi la madhehebu fulani, bali kutumikia Neno Lake. Hivyo ndivyo. *Hao ni Roho Wake watumikao, waliopelakwa.*

Tunajuaje wamepelekwa? Biblia ilisema kwamba, "Neno la Bwana liliwajia manabii." Hiyo ni kweli? Malaika hawa huhudumu Neno Lake, kwa Roho Wake; kuhudumu Neno kwa Roho Mtakatifu. Na Roho na Neno viliwajia manabii; nao manabii walikuwa na Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu wangeweza kufanya miujiza waliyofanya. Haikuwa mtu yule; ilikuwa ni Roho wa Mungu ndani ya mtu huyo. Roho wa Kristo ndani ya mwanadamu, kwa ajili ya Neno la Mungu. Alikuwa amefanya nini? Kusafishwa kila mkondo. Mungu alikuwa amemchagua, naye alikuwa ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Wala haikuwa ni yeye. Yeye hakutenda neno mpaka alipoliona kwenye ono. Eliya alisema Mlimani Karmeli, "Yote haya nimeyatenda kwa amri Yako. Sasa, Bwana, na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu." Loo, utukufu kwa

Mungu!

95 Nimeliona mara nyingi sana, unapooni Roho wa Mungu akishuka mahali fulani, na mahali hapo pakawa chini ya upako! Kama kundi hili dogo hapa asubuhi hii, lingeweza tu kuchukua akili hii hapa, liondolee mbali kila shaka! Unawezaje kutilia shaka tena, wakati unapooni wafu—wafu wamefufuka, viwete wakitembea, vipofu wakiona, viziwi wakisikia?

96 Malaika wa Bwana, hata picha Yake inaning'inia hapa kwenye ukuta, imeitia mshangao sayansi kila mahali. Yeye anafanya nini? Dumu moja kwa moja na Neno. Amina! Hukata kila pepo. Ndiyo, linakata. Ni kitu gani? "Roho zinazowahudumia, zilizotumwa kutoka Mbele za Mungu," kuwapaka mafuta wale wanenaji wa Neno, ambao hudumu na Neno. Naye analithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata, anamleta Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele. Huyu hapo.

Tungewezaje kushuku, wakati Yeye yuko kisayansi, kimwili, kiroho, kila njia inayoweza kuhakikishwa, Yeye amehakikishwa hapa?

Kuna nini? Ni katika akili zetu. Tunafungua akili zetu kwa jambo hilo, tuseme, "Vema, sasa, sijui kama ingewezekana au la. Labda, kama nikijisikia vizuri kesho." Loo, hilo halina uhusiano wowote nalo.

97 Kama nilivyosema mara nyingi, huenda Ibrahimu alimwambia Sara ... Alikuwa amepita umri wa—wa kuwa mwanamke. Mnajua ninalomaanisha; wakati wake wa maisha, siku zake ishirini na nane. Mnaona, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Pengine alikuwa amepita, kwa miaka kumi na mitano, ishirini Naye akamwambia, labda, siku chache zilizofuata, akasema, "Unajisikia tofauti yo yote, mpenzi?"

"Hata kidogo."

"Hilo halina uhusiano wowote nalo. Tunaendelea mbele, kwa vyo vyote. Vema sasa, ukianza kurudi kama mwa—mwanamke kijana tena, tunajua, hilo kwa damu hiyo ya uhai, vema, basi, tunaona hapo kwamba itamfanyia makazi mtoto mchanga, na kila kitu kitakuwa sawa. Sasa, unajisikia tofauti yoyote leo? Imekuwa mwezi mmoja tangu aliponiahidi. Unajisikia tofauti, mpenzi?"

"Hata kidogo, Ibrahimu. Hakuna hata dalili, hakuna kitu. Ni—ningali ni kama tu vile nilivyokuwa sasa kwa miaka michache iliyopita. Hakuna tofauti hata kidogo."

"Utukufu kwa Mungu! Tutampata, haidhuru."

98 "Unamaanisha, Ibrahimu, juu ya ... Angalia, kama Yeye alikuahidi, hakika Yeye angetupa ishara namna hii. Hakika Yeye angetupa ishara." A-ha! Haleluya!

"Kizazi kinyonge na cha zinaa chataka ishara." Hiyo ni kweli. Alikuwa na ishara. Ilikuwa ni kitu gani? Neno la Mungu. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara.

Mungu angewezaje kumponya mtoto huyu? Neno la Mungu lilisema hivyo; kama nikisikia msisimko, ama sina msisimko. Kama mimi ... Haidhuru ni jambo gani linalotukia, Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.

99 Ibrahimu alisema, "Kusanyeni kofia zenu na kila kitu pamoja, tunaenda zetu kwenye ile nchi."

"Mnaenda wapi?"

"Mimi sijui." Amina. "Lakini, tunaenda, vyo vyote vile. Haya twendeni!" Walifungasha na kuondoka. Haleluya! Hilo ni Neno halisi la Mungu. Alishikilia nini mbele yake? Ahadi ya Mungu, Neno la Mungu. "Tutampata."

100 "Toka miongoni mwa watu wako, Ibrahimu. Wao ni, jambo ni kwamba, wao ni wenye kushuku na wasioamini. Wao watakutia kwenye mashaka hayo hayo. Njoo huku nje. Toka ukajitenge nao, uniishie Mimi." Ni kitu gani? "Acha dhamiri yako yote na hisi nyuma yako, namna hiyo. Fungua akili yako, na ukumbuke, ni Mimi. Njoo, ukaishi pamoja Nami." Amina.

Mungu anaita kila Mzao wa Ibrahimu, asubuhi ya leo, kwenye maisha ya aina hiyo. Vita vikuu vinaendelea sasa, ulimwenguni mwote. Mungu anataka watoto Wake wajitenge na kitu gani? Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia; mawazo, dhamiri, kumbukumbu, hoja, upendo; kila kitu. Wafungue akili zao waruhusu Neno liingie ndani na watembea pamoja na Neno. Huyu ni askari halisi.

101 Hivyo ndivyo nyota zinavyosimama. Mfumo wa jua haujabadilika; ile zodiaki. Ile nyota ya asubuhi inachomoza kwenye wajibu wake, kila asubuhi, jinsi hasa ilivyofanya wakati dunia ilipoumbwa. Ile nyota ya jioni inachukua mahali pake; kila nyota. Kundi dogo la nyota, katika majira yake, lipo pale pale tu linapopaswa kuwa. Nyota ya Kaskazini inasimama imara na haitembea kamwe. Haleluya! Jambo hilo lote linaizunguka Nyota ya Kaskazini, hizo zingine zote, kwa sababu iko moja kwa moja katikati ya dunia.

102 Huyu ni Kristo. Amina. Yeye anasimama pale, anaamuru jeshi Lake kama Kapteni mkuu.

Kama vile Musa mlimani huku ameinua mikono yake juu, na Israeli walikuwa wakipigana, wakikatiza njia, naye akasimama ameinua mikono yake juu. Alisimama ameinua mikono yake mpaka jua lilipotua. Iliwabidi waishikilie mikono yake juu. Huyu alikuwa ni Musa.

Alikuwa mfano wa Kristo. Ili kuhakikisha kwamba mikono Yake inakaa juu, mikono Yake ilipigiliwa misumari msalabani. Haleluya! Naye akapanda ngome za Utukufu, leo, akiwa na mavazi Yake yenye Damu mbele za Mungu, kwenye mkono wa kuume wa Ukuu Wake Huko. Na vita, kwa kila askari, atafyeka afanyize njia. Mimi sijali nini kitakachotukia; kwa Neno la Mungu, atakata hata ajiweke huru. Amina.

103 Kama vile kifaranga katika yai, itakuwaje kama yeye anaogopa kutoboa? Vipi kama anaogopa kutoboa yai? Vipi kama huyo kifaranga mdogo ndani ya yai, ndege mdogo, aliogopa kugongagonga ganda la yai? Vipi kama angesikia sauti kutoka nje, ikisema, "Usigonge ganda hilo; huenda ukajiumiza mwenyewe"? Bali asili yenyewe, katika ndege yule, inamwambia, "Lidono! Toboa tundu katika hilo."

Hebu madhehebu yote ya kale yasema, "Siku za miujiza zimepita. Utajiumiza. Umeanza kuwa shupavu wa dini."

Donoa ganda, kwa nguvu uwezavyo. Haleluya! "Shetani, ondoka! Ninatoka humu ndani." Ndivyo hivyo. "Silali hapa, tena. Sikai hapa, tena Mimi siko kwenye ardhi hii ya ibilisi ya kale tena. Ninadonoa nipate njia ya kutoka, asubuhi hii. Amina. Mimi ni tai." Amina! Haleluya!

104 Lakini maskini yule tai wa kale, mwenye shingo la kijinyundo nyuma kule, akidonoa kwenye ganda lile. Haidhuru ganda lile lilikuwa ni gumu vipi, alilidonoa akalitoboa kabisa. Jambo la kwanza unajua, basi, angeweza kupigapiga mabawa yake kidogo. Yeye alikuwa mzima.

Donoa utoke. Hiyo ni kweli. Unalifanyaje? Kulilipua kwa "BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI. BWANA ASEMA HIVI." Hatimaye, unaanza kunusa hewa safi. "BWANA ASEMA HIVI." Umetokeza kichwa chako nje. "BWANA ASEMA HIVI." Sukuma kwa nguvu sasa, unatoka!

Yeye harudi kwenye ganda tena. Amina. Yuko huru. Loo, jamani! Neno lile likisha tu kuwekwa chini, kupitia hisi hizo zote na dhamiri, na kadhalika, hadi Hili litulie chini *hapa*, na akili hiyo inafunguka na kuliruhusu. Ee Mungu, uturehemu! Hakuna kamwe kitu cha kumtia utumwani tena. Uko huru. Yeye ambaye Mwana amemfanya huru ametoka kwenye ganda. Madhehebu yako kamwe hayawezi kukuita urudi. Ibilisi hangeweza kukufanyia jambo lolote zaidi. Yeye anakufanyia mlio wa nyoka na kukuzomea, basi.

105 Lakini uko kwenye njia kuu, ukikimbia kasi, loo, jamani, ukikimbia kwenye njia kuu ya Mfalme, askari aliyetiwa mafuta wa msalaba. Enyi tai wote, mlio na imani, mtangazeni Yesu, Nuru ya ulimwengu, kimbieni katika njia kuu ya Mfalme. Hakika. Naam, bwana!

106 Hawa ni "Roho watumikao" waliopolekwa toka Uweponi mwa Mungu, kuwa wahudumu, kuhudumu (nini?) Neno Lake; siyo theolojia fulani, bali Neno la Mungu. Wao ni Roho watumikao, waliotumwa kutoka kwa Mungu, kuhudumu. Roho watumikao! Loo! Basi kumbuka, kama akihudumu kitu fulani kando ya Neno, hakutoka kwa Mungu. Maana, "Neno Lako daima limethibitishwa Mbinguni." Sikuzote Mbinguni, Neno, Mungu huliangalia Hilo. Naye kamwe hatamtuma roho kuhudumu kitu kingine mbali na Neno.

Kamwe hatamtuma roho aliye na D.D.D., Ph.D. kubwa, na ukosi wake umegeuka nyuma, kila kitu namna hiyo, aseme, "Vema, bila shaka, siku za miujiza zimepita. Sote tunajua jambo hilo." La, la. Hilo halikutoka kwa Mungu. Ni kinyume cha Neno. Amina.

Yeye huwapeleka wale ambao huhudumu Roho wa Neno. Amina.

Loo, nilikuwa na vitu kama vinne ama vitano zaidi, lakini nitaviacha vipite wakati huu, nitavichukua Jumapili ijayo. Vema.

Shetani na pepo wake wametiwa mafuta.

107 Kama Roho hizi za malaika zimetiwa mafuta kuwaleteeni Neno, kuwafanya muamini Neno, sasa, umepata kuona ambapo umewahi kusikia nabii, nabii halisi wa Mungu akikana Neno la Mungu? [Kusanyiko linasema, "La." — Mh.] La, bwana. Ni nini kilichotukia wakati madhehebu ya siku zao yalipoinuka na kusema, "Sasa, amekosea"? Alisimama mwenyewe, na kusimama peke yake. Akasema, "Ni kweli."

108 Mwangalie Mikaya kule chini siku ile, maskini mtakatifu anayejifingirisha, mnaona, mwana wa Imla. Kulikuwako na mia nne waliotiwa mafuta, walidhaniwa kuwa, manabii waliotiwa mafuta wamesimama pale, wote wamelishwa vizuri, na kuwekwa vizuri, na shahada kubwa, na wasomi wenye elimu na wanachuoni walioadibishwa. Kasema, "Kwea, mfalme wetu mwaminifu. Bwana awe pamoja nawe. Hiyo ni yetu. Yoshua alitupa sisi. Kwa hiyo kwea ukaitwae. Hiyo ni kweli kabisa. Kwea ukaitwae. Nini ..." Akasema, "Vema, Yosh- ..."

Unajua, Yehoshafati akasema, "Je! hayupo mwingine mahali fulani?" Vema, walikuwa na mia nne. Kwa

nini asiamini wale mia nne? Akasema, "Lakini hakika, mna mwingine mahali fulani."

Kasema, "Mimi—mimi ... Vema, tuna mmoja. Kuna mwingine, lakini, loo, ninamchukia." A-ha! Mnaona?

"Papo—hapo, huyo ndiye jamaa ningetaka kumsikiliza, mnaona." Kasema, "Mleteni. Hebu tuone atakalosema."

109 Na kwa hiyo wakaenda wakamwambia, wakasema, "Sasa, sikiliza. Wewe panga mahubiri yako barabara, asubuhi hii, sababu unamhubiria mfalme. Unahubiria cha ... chama cha wahudumu wa *Fulani na fulani*, mnaona, wa Palestina, chama chote cha wahudumu. Naam, kumbuka, hivi ndivyo walivyosema. Wewe nena jambo lile lile. Amini jambo lile lile." Maskini huyo...

Yeye—yeye alikuwa na mtu asiyestahili pale. Mtu yule aliisha achana na akili hii ya kale yenye kuhoji. Alikwisha safisha lile bomba, mnaona, dhamiri yake.

"Na, vema, mbona, unajua watakalofanya? Kama utasema jambo lile lile, nafikiri watakufanya mkuu wa wilaya. Labda watafanya hivyo. Wata—watakufanya mwangalizi wa mambo yote ya humu wilayani kama uta—kama utakubaliana nao." Huyo hakuwa mtu halisi wa Mungu.

Mbona, mabomba yake yalikuwisha safishwa, dhamira zake zote na kila kitu wazi. Akili yake ilikuwa imefunguliwa kwa Neno la Mungu. Na Neno la Mungu, tu, angeamini. Hao ni Roho watumikao. Huyo ni Roho atumikaye.

Akasema, "Sijui niseme nini sasa. Lakini, nitawaambia jambo hili moja, nitasema tu yale Mungu anayoniambia niseme."

Kwa hiyo wakangojea usiku huo. Alikuwa na ono.

110 Kesho yake asubuhi, naweza kuwazia Mikaya akiyachunguza Maandiko na kusema, "Sasa, hebu tuone sasa. Hivi ono lile... Naam, watu hao wote, kuna kasoro fulani mahali fulani hapa, sababu ni kinyume cha walilolisema. Bali, lingesema nini Hilo? Hebu tuone kile Eliya alichosema nyuma hapa, yule nabii, maana tunajua alikuwa nabii. Angalia kile ... Neno la Bwana lilimjia Eliya. Naam. Nalo lilisemaje? 'Na mbwa watailamba damu yako. Yezebeli, mbwa watamla. Na kwa sababu ya Ahabu mwenye haki ... Nabothi mwenye haki.'" Alisema basi ... Wakati alipoona jambo hilo, aliona ya kwamba ono lake lilikuwa sawa tu na Neno la Mungu, basi, huyo mzee Ahabu alikuwa amemjia.

Aliondoka akaenda hadi pale akasema, "Kwea, bali nimeona Israeli..." Mnaona, yeye hakuona aibu kusimulia ono lake wakati huo, maana lilikuwa ni Neno la Bwana. Alijua angeweza kuchukua kitu hicho kikamilifu kabisa. Nini? Alikuwa ameufungua moyo wake, na akili zake kwa Neno la Mungu, na Neno la Mungu lilikuwa limeisha kufunuliwa kwake, kwa hiyo alijua hilo lilikuwa Neno la Mungu kikamilifu.

111 Sasa, unasema, "Loo, laiti ningaliweza tu kuwa Mikaya!" Unaweza kuwa. Ndivyo ulivyo. Ndivyo ulivyo pia, Mpenzi. [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] Wewe ni Mikaya, nabii. Unaweza kufanya nini? Fungua akili yako. Ninajaribu kuwaambia nini asubuhi ya leo? Neno la Bwana. Mnaona? Fungua akili yako, useme, "Sasa, mnajua, ninaamini ninaweza kuponywa." Vema, ni kitu gani, basi? Je! Ni Neno la Bwana? Hakika, ni Neno la Bwana.

Na jamaa huyu *hapa* anasema, "Siku za miujiza zimepita. Huwezi kufanya jambo *hili*. Na wewe ..." Sahau kuhusu jambo hilo. Mtangulize Mungu.

Hili hapa Neno la Bwana linakuja, naye alilinena, Nalo likawa.

112 Sasa, Shetani alifanya nini? Shetani aliwatia mafuta wale wengine. Naam, Shetani hutia mafuta watumishi wake. Loo, hakika. A-ha. Hakika. Yeye huwatia mafuta watumishi wake. Anawatia mafuta kwa kitu gani? Na kutokuamini. Shetani na pepo zake huwapaka wanadamu mafuta wasiliamini Neno la Mungu.

113 Sasa, kama unataka kuthibitisha jambo hilo, fungua Mwanzo 3:4. Hebu na turudi nyuma tu hapo na tusikilize hili, kwa dakika moja tu, na tuone kama hiyo si mbinu yake ya kwanza. Hilo ndilo jambo la kwanza alilofanya. Yeye kamwe haachi mbinu zake zile zile. Yeye hufanya hivyo wakati wote. Sasa, angalia tu kama hiyo—hivyo ndivyo ilivyo. Sasa, hakulipinga Neno. Kwa namna fulani alimfanya aelewe hilo vibaya kidogo tu, mnajua, kwa namna fulani kulifanya Hilo lisikike jinsi alivyolitaka Hilo lisikike, usichukue Neno zima. Sasa, Mwanzo, nimepata hapa, Mwanzo 3:4. Hebu tuone kama hivyo ndivyo linasema sasa. Vema.

*Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa:*

*Hakika hamtakufa.*" Mnaona jinsi alivyolinukuu vinginevyo? "Loo, tunaamini siku za miujiza zimepita. Hatuamini kuna kitu kama watu wanaompokea Roho Mtakatifu kama walivyompokea Pentekoste. Loo, kwa vyovyote unavyobatizwa, haileti tofauti yoyote." Mnaona ibilisi? Mnaona mbinu zake? "Vema, kama daktari alikuambia huwezi kupata afya, hilo latosha."



114 Naam, si kumvunjia heshima, kutokumwamini daktari. Daktari anatenda kazi katika njia ya kisayansi. Naye daktari amefanya kila awezalo, kuokoa maisha ya mtu huyo. Na hayawezi kuokolewa, kwa sababu hakuna kitu kingine ajuacho kutenda. Amefikia kikomo cha akili zake. Mtu huyo ni mwaminifu. Lakini, sasa, ule mti wa maarifa ni sawa, bali unapofikia kikomo chake, basi nenda kwenye Mti wa Uzima na kusonga mbele. Amina. Hivyo ndivyo ilivyo. Itafanya tu kazi umbali huo. Naam.

Sasa, mbinu ya Shetani ni nini sasa? Yeye alisema nini hapa? Sasa angalia kifungu cha 1 na cha—cha 2. Sasa hebu—hebu nisome kifungu cha 1 hapa, hadi 3.

*Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wote—wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile...matunda ya miti yote ya bustani?*

115 Msikilize sasa, jinsi tu anavyochukiza na jinsi yeye—jinsi anavyolipaka hilo Neno chokaa. Mnaona? Yeye ni ... Yeye anajaribu kufanya nini? Ingia moyoni mwake. Mnaona? Yeye anazungumza naye, baada ya Neno tayari kuimarishwa pale.

Sasa, usimwachilie Shetani afanyie ngome cho chote. Mnaona? Wewe lifanye ngome Neno la Mungu moyoni mwako. Mnaona? Unafanya vivyo hivyo. Sasa angalieni, enyi akina Mikaya.

*... Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; bali ...*

*Lakini matunda ya mti ulio katikati (katikati, mnaona) ya bustani, Mungu...amesema, Msiyale, wala msiyaguse, msije mkafa.*

Mnaona, sasa, hilo ni Neno. Anamnukuulia hilo. Sasa angalia.

*Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa:*

116 Mnaona mbinu yake? Mnaona? Yeye anajaribu kufanya nini? Yule mwanadamu wa kwanza, anajaribu kumtia mafuta yule mwanamke wa thamani pale, binti wa Mungu, kwa kutokuamini katika Neno la Mungu. Hivyo ndivyo hasa anavyojaribu kumfanya afanye.

Hivyo ndivyo anavyojaribu kukufanya ufanye, mpenzi. [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] Hivyo ndivyo anavyojaribu kumfanya kila mmoja wenu afanye, huko nje, awatie mafuta. Na jambo pekee unalopaswa kufanya sasa ... Wewe ni mtu mwenye hiari ya kuchagua. Sasa unaweza kulikubali ukitaka. Lakini lipige teke. Laiti Hawa asingalisimama muda ule, kusikiliza! Usisimame kamwe. Usisimame.

117 Wakati—wakati Eliya alipomwambia Gehazi, aliposema, "Chukua fimbo yangu, nenda ukaiweke juu ya mtoto aliyekufa. Na kama mtu ye yote akinena nawe, usimjibu. Kama ye yote akijaribu kukuzuia, endelea tu."

Mwangelie yule mwanamke wakati alipomwita mtumishi wake. Alisema, "Jitandikie nyumbu unitangulie, na hata usisimame mpaka nitakapokuambia." Hivyo ndivyo ilivyo.

Ukiwa na Ujumbe, endelea mbele. Amina. Sema, "Siwezi kutembea tena. La, ninakuwa mdhaifu." Endelea tu mbele. Usisimame. Ukiweka kando kila kitu, endelea kufyeka upate njia. Ndugu, una Upanga mkononi mwako, endelea tu kukata.

118 Nilikwenda kwenye uwanja wa mpira, wakati mmoja, na nilikuwa naenda kuhubiri. Nami nikasimama mlangoni na kuangalia juu, kule juu. Kuliandikwa, "Si ukubwa wa mbwa katika mapambano. Ni ukubwa wa mapambano katika mbwa." Kwa hiyo hicho ndicho kinachoshinda vita. Mnaona?

Unasema, "Vema, angalia. Angalia makanisa yote makuu yanapinga jambo Hili."

Sijali wana ukubwa gani. Ni lile pambano ambalo limo ndani ya mbwa, hilo ndilo lenye maana. Ni imani iliyo ndani ya mtu binafsi. Kama wewe u mwoga, rudi tunduni ukajikunyate. Lakini, ndugu, kama wewe ni askari, simama pale. Vita vinaendelea. Kweli na uongo vinapambana. Hebu tupigane.

119 Kama Peter Cartwright alivyoingia katika jiji fulani, akasema, "Bwana aliniambia mimi ni—nije hapa na kuanzisha ufufuo." Akakodi stoo ya zamani, akaingia humo, akaanza kuisafisha.

Basi jitu moja katili la lile jiji, huku bastola inaning'inia ubavuni mwake, lilishuka. Likachukua milango ... Baadhi yao, walisema, "Jamaa huyo anafanya nini kule chini?"

Kasema, "Yeye ni mhubiri. Yeye atakuwa na mkutano, alisema."

"Vema," akasema, "nadhani itanibidi kushuka tu na kumtupa nje barabarani, na kumfukuza hapa. Hivyo tu. Hatutaki mikutano yo yote karibu na mahali petu."

120 Hivyo anashuka anaenda huko, na kusimama mlangoni. Naye Peter Cartwright alikuwa amevaa koti

lake, mwajua, naye alikuwa akiosha tu madirisha na kuta chini. Jamaa mdogo sana, mwajua.

Yule mhubiri wa zamani alimcheka, mnajua, kwa kula kuku kwa mikono yake; jambo ambalo ni kawaida leo, mnajua.

Kwa hiyo alikuwa tu anasafisha madirisha na kutengeneza kila mahali. Lile jitu katili likamwendea, likavuta nyuma koti lake, huku bastola imening'inia ubavuni mwake, kasema, "Unafanya nini?"

"Loo," akasema, "ninasafisha madirisha." Aliendelea tu kusafisha madirisha, mnajua. Alikuwa na kusudi moja. Mungu alimwambia afanye uamsho. Akaendelea, kusafisha madirisha.

Akasema, "Sisi haturuhusu uamsho hapa."

121 Akasema, "Loo, lakini Bwana aliniambia ku—kufanya uhamsho huu." Mnaona? Aliendelea tu, kujishughulisha na kazi yake. Mnaona? Mnaona?

Akasema, "Kuna jambo moja linalokupasa—linalokupasa kufahamu." Akasema, "Mimi ndiye ninayetawala mji huu hapa."

Akasema, "Loo, kumbe ni wewe unautawala?" Naye aliendelea tu kusafisha madirisha, mnajua.

Akasema, "Kabla ya kufanya ufufuo itakubidi unichape unishinde kwanza!"

Akasema, "Kumbe, inanibidi nikuchape? Vema, nitafanya hivyo baadaye."

Yeye alivua tu koti lake. Akaenda akamshika ukosini, akamtupa chini sakafuni, kisha akamrukia na kumkalia. Akasema, "Sharti nipigane vita nipate kutawala. Niongezee ujasiri, Bwana." Akamtwanga akaona kilichomtoa kanga manyoya.

Kasema, "Je! Umetosheka?"

Akasema, "Naam." Akaamka na kumpa mkono. Yeye aliokolewa usiku huo, kanisani.

122 Haya basi. Mnaona? Chukua tu Neno la Mungu ufyeye upate njia kupitia kila shaka. Mnaona? Hakika, ndivyo ilivyo. Hiyo ndiyo kazi inayofuata, hebu na tuifanye. Sawa. Jambo la pili ninalopaswa kufanya ni kuondoka kwenye mashaka yangu, kuyakatalia mbali. Hiyo ndiyo kazi yangu, inayofuata ni kuondoa mahangaiko yangu. Kama hisi zangu zikiniambia, "Naam, wewe unaumwa," jambo la pili ni kukatilia kitu hicho mbali. Hiyo ni kweli.

Unasema, "Vema, wewe ... Wananiambia ya kwamba ... Unajua, dhamiri yangu yaniambia, Ndugu Branham, kwamba mimi..." Vema, afadhali ukatilie mbali jambo hilo. Hutaenda mbali zaidi ya hapo. Fanya tu kazi yako inayofuata. Vua koti lako ukajiingize moja kwa moja kazini. Endelea tu kusonga mbele. Kusudi moja, "Nitashinda." Amina. "Siwezi kupoteza. Nitashinda." Amina.

123 Shetani hutia mafuta. Mnaona? Mbinu yake ya kwanza ni nini? Mahali pake pa kwanza kupafikia palikuwa ni wapi? Akilini. Mwanamke alisimama kwa muda kidogo, kusikiliza alilosema. "Loo, usiseme hivyo?"

Hapo ndipo ambapo maskini wanawake wengi walipofanya makosa yao, na maskini wanaume wengi walifanya makosa yao; hilo ni kweli, kusimama kidogo, kusimama tu kidogo. Mara ngapi nimeona kesi za talaka na mambo kadha yakizuka, kwenye hilo.

124 "Naam, nakuambia, Ndugu Branham, alipiga mruzi kama 'wiiti-whiu', mnajua, nami nikasimama; na kwa kweli, si—sikukusudia." A-ha. Haya basi.

"Loo, yeye, nilikuwa nimeketi upande wa pili wa meza kutoka kwake. Yeye—mwanamke alikuwa na macho mazuri kupindukia!" Mnaona? A-ha. Mnaona? Ndivyo hivyo.

125 Ibilisi hufanya jambo lile lile. "Loo, daktari aliniambia singeweza kupona, kwa hiyo mimi ..." Haya basi, jambo lile lile, mnaona, vita vikubwa sana vilivyowahi kupigwa.

"Vema, wananiambia ... Nilimwona *Fulani* akidai kuwa na Roho Mtakatifu." Naam, mlimwangalia maskini mnaofiki fulani. Je! vipi kuhusu hao ambao kweli wanaye Huyo? A-ha. Naam. Ibilisi atakuonesha maskini chambo fulani cha kunguru, bali hatakuonesha hua halisi. A-ha. Hiyo ni kweli. Hatakuonesha huyo; atakupofusha usije ukamwona.

Loo, yeye ni shujaa, pia, kumbukeni. Lakini mkuu ni ninii yetu ... "Aliye mkuu zaidi ni Yeye aliye ndani yako, kuliko yeye aliye katika ulimwengu." Kwa hiyo shikilia Neno la Mungu; liamini Hilo; enyi makapteni wa jeshi hapa. Shikilia ngome yako, ndugu. Hiyo ni kweli, shikilia jukumu lako.

126 Kwa hiyo, nilikuwa na msichana mdogo hapa, wakati mmoja. Huenda mwanamke huyo ameketi hapa sasa. Jina lake lilikuwa Nellie Sanders. Mojawapo ya mara za kwanza nilizowahi kuona pepo akitolewa.

Tuliishi, sasa, kama ninaweza tu kupapata mahali pale; na ingekuwa kama tu majengo matatu juu hapa, kupita makaburini. Na mimi ilikuwa ndiyo kwanza niwe mhubiri, nami nilikuwa nahubiri kwenye mkutano, wa hema papa hapa pembeni.

Na maskini msichana huyo alikuwa mmoja wa wacheza dansi hodari sana. Alienda shule ya sekondari hapa chini, na yeye na Lee Horn. Na wengi wenu hapa mjini mnamjua Lee Horn hapa chini, anaendesha chumba cha kuchezea kamari kule. Na kwa hiyo wao, yeye na Lee Horn, walikuwa wacheza dansi bora sana waliokuwepo nchini. Yeye ni Mkatoliki, yeye mwenyewe. Bila shaka, dini haikumaanisha kitu kwao, kwa hiyo basi ... Nellie na hao wengine. Kwa hiyo, yeye alikuwa mcheza dansi hodari, naye alikuwa, pia. Nao walikuwa na dansi hii hapa inayoitwa "kitako cheusi," na "ngoma kasi," na mambo hayo yote. Naye alikuwa ... Hao wawili ndio waliokuwa bora sana nchini.

127 Siku moja alipepesuka akaingia humu, usiku mmoja, mkutanoni. Hapo akaanguka chini, madhabahuni, maskini Nellie. Mungu aubariki moyo wake. Alilala pale madhabahuni. Aliinua kichwa chake. Naye akalia, na machozi yakitiririka mashavuni mwake. Akasema, "Billy ..." Alinijua. Akasema, "Nataka sana kuokoka."

Nami nikasema, "Nellie, unaweza kuokolewa. Yesu tayari amekuokoa, ewe msichana. Yakupasa uukubali sasa juu ya msingi wa Neno Lake."

Naye akakaa pale. Naye akalia, naye akaomba, naye akamwambia Mungu asingeyasikiliza mambo ya ulimwengu tena. Mara, amani nzuri sana ikaingia nafsini mwake. Akainuka kutoka hapo, akipiga makelele na kumsifu Mungu, akimtukuza Mungu.

128 Na yapata miezi sita ama minane baada ya hapo, alikuwa akishuka kuja kwenye Barabara ya Spring, usiku mmoja.

Sasa, akiwa msichana mdogo, alikuwa tu katika umri wa tineja, kama miaka kumi na minane. Naye akanijia, na kusema, "Natumaini ..." Huyo alikuwa ni mke wangu, yule aliyeaga dunia. Akasema, "Laiti ningalionekana kama Hope na Irene." Akasema, "Unajua, hawakuingia kamwe katika mambo ya ulimwengu." Kasema, "Ulimwengu unakutia alama." Kasema, "Nilipata sura ya kijeuri." Kasema, "Sasa niliacha kujipodoa na kadhalika, bali nina sura ya kijeuri. Hata sura ya uso wangu," akasema, "mimi naonekana jeuri." Akasema, "Wanaonekana wasio na hatia na wapole." Kasema, "Laiti nisingalifanya jambo hilo kamwe."

Nikasema, "Nellie, Damu ya Yesu Kristo husafisha dhambi zote, mpenzi. Nenda zako, liamini."

129 Wayne Bledsoe, wengi wenu mnamjua hapa, rafiki yangu wa moyoni, kwa miaka kadha wa kadha. Alikuwa mlevi. Naye akaja hapa pamoja na ndugu yangu, Edward. Naye akanywa kule chini mtaani, nami nikamchukua, kwa sababu polisi walikuwa wanataka kumchukua. Nami nikamleta hapa. Nami nilikuwa mhubiri na niliishi hapa, mama na baba yangu, kabla sijaoa. Nami nikamchukua, nikamweka kitandani mle. Nililala, nililala kwenye kitanda cha watu wawili cha mkunjo. Kulikuwako na kundi kubwa la Branham, mnajua, tuko kumi. Na kwa hiyo tulikuwa na kama vyumba vinne, na ilitubidi kwa namna fulani tulale wawili-wawili, kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa na kitanda cha watu wawili cha mkunjo nilicholalia. Nami nilikivuta nje hivi, na—na kumweka Wayne kitandani alale pamoja nami, amelewa. Akiwa amelewa, ilibidi nimbebe humo nyumbani na kumlaza kitandani.

Nami nilikuwa nimelala pale. Nikasema, "Wayne, hivi huoni aibu ukiwa namna hiyo?"

130 Naye akasema, "A-ha, Billy, usinizungumzie namna hiyo." Na ndipo nikaweka mkono wangu juu. Nikasema, "Nitakuomba, Wayne. Mungu akubariki." Nami nilikuwa nimeokolewa karibu, loo, nadhani karibu, labda mwaka mmoja.

Na kwa hiyo basi, mara moja, te—tekisi, ikafungwa mlango huko nje, na mtu akapiga hodi kwa nguvu sana. "Ndugu Bill! Ndugu Bill!" [Ndugu Branham anagonga mimbara — Mh.]

Nikawaza, "Jamani, lahaua, lazima kuna mtu anayekufa." Nikaruka, kwenda mlangoni, nikanyakua kitu changu kikuukuu pale, nikakizungusha kwenye pajama zangu namna hii, nikamfunika Wayne. Nikakimbilia mlangoni.

Ilisikika kama mwanamke. Nikafungua mlango, na huyu msichana mdogo amesimama mlangoni. Akasema, "Loo, naweza kuingia?"

Nikasema, "Ingia." Nami ninawasha taa.

Na sasa, alikuwa akilia namna hiyo, akasema, "Jamani, Bill—Billy, nime—nime—nimekwisha. Nimekwisha!"

131 Nikasema, "Kuna nini, Nellie? Umepata u—ugonjwa wa moyo?"

Akasema, "La." Akasema, "Ndugu Bill, nilikuwa nikishuka kuja Spring." Akasema, "Kweli, Ndugu Bill!

Kweli, Ndugu Bill, sikukusudia mabaya. Sikukusudia mabaya;

Nikasema, "Kuna nini?" Nikawaza, "Nitafanya nini naye sasa?" Sikujua la kufanya. Nilikuwa, tu kijana. Nami ...

Kasema, "Loo, Ndugu Bill," kasema, "niko tu—niko tu—nimechanganyikiwa kabisa."

Nikasema, "Sasa, tulia, dada. Niambie yote kuhusu hilo."

Naye akasema, "Vema," akasema, "nilikuwa ninashuka kuja barabarani, na Ukumbi wa Redmen..." Basi walizoea kuandaa dansi ya Jumamosi usiku kule. Naye akasema, "Nilikuwa na kitambaa; nilikuwa ninaenda nyumbani kujishonea nguo." Naye akasema, "Nilisikia muziki huo." Naye akasema, "Unajua," kasema, "nilisimama kwa dakika moja tu." Akasema, "uliendelea kuwa mzuri. Kwa hiyo nikawaza, 'Unajua, haitadhuru kama nikisimama papa hapa."

132 Hapo ndipo alipofanya kosa lake, akasimama kwa muda kidogo. Yeye alisikiliza tu.

Kasema, "Vema, nitafikiria." Kasema, "Ee Bwana, unajua nakupenda, hata hivyo." Kasema, "Unajua nakupenda, Bwana. Lakini ninaweza hakika kukumbuka wakati ambapo mimi na Lee tulikuwa tukichukua vi—vikombe vyote na kadhalika." Kasema, "Jamani, ninakumbuka muziki ule wa kale ulikuwa unanivutia. Sasa haunivutii."

Loo, loo! Unafikiri tu haukuvutii, Tayari umekwisha kukushika, papo hapo. Hilo ni sawa tu na anavyotaka papo hapo. Mnaona?

Ni wangapi waliopata kumjua Nellie Sanders? Vema, nadhani wengi wenu. Naam. Hakika. Kwa hiyo wao—wao walikuwa—walikuwa ...

Kasema, akasema, "Vema, unajua nini?" Kasema, "Labda nikienda kwenye vipandio kule," kasema, "labda nitaweza kuwashuhudia baadhi yao."

Loo! Mnaona, uko moja kwa moja kwenye uwanja wa Ibilisi. Kaa mbali nalo. Epuka tu kule kuonekana kwa uovu."

Lakini yeye alipanda, juu ya vipandio, akasimama pale dakika chache. Na muda si muda unajua, alikuwa amemkumbatia mvulana fulani, huko nje sakafuni.

Ndipo akajirudia. Naye alikuwa amesimama pale, akilia na kuendelea, akasema, "Loo, nimepotea sasa, kabisa."

133 Nikawaza, "Vema, sijui mengi sana kuhusu Biblia, bali ninaamini Yesu alisema hivi, 'Katika Jina Langu watatoa pepo.'" Mimi ...

Naye Wayne alikuwa amekomaa, kidogo, naye alikuwa ameketi pale, akitazama. Mnaona? Kwa hiyo nikasema, "Sasa, ibilisi, sijui wewe ni nani, bali ninakwambia sasa, huyu ni dada yangu, nawe huna haja ya kumshikilia. Yeye hakumaanisha kufanya hivyo. Alisimama tu kwa dakika moja." Hapo ndipo alipofanya kosa lake, hata hivyo. Nikasema, "Lakini itakubidi utoke kwake. Unanisikia?"

Na kwa hiyo nisaidie, Mungu, atajua kwenye kiti cha hukumu. Huo mlango wa kioo ulianza kufunguka na kufunga, wenyewe. "Plampiti, plampiti," pale mlango. "Pumpu, ka-plampu, ka-plampu." Nikawaza.

Naye akasema, "Bill, angalia pale. Angalia kule."

Nami nikasema, "Naam. Ni kitu gani hicho?"

Akasema, "Sijui."

Nikasema, "Wala mimi pia."

134 Nao mlango ukaenda "pampiti-pampu, ti-pampu," ukijifunga namna hiyo. Nikawaza, "Kuna nini hapa? Kuna nini?"

Nikaangalia tena, namna *hiyo*. Nikasema, "Mwache, Shetani! Katika Jina la Yesu, mtoke!"

Niliposema hilo, ilionekana kama popo mkubwa mno, yapata urefu *huu*, aliruka kutoka nyuma yake, akiwa na nywele ndefu zikining'inia chini toka kwenye mbawa zake na kwenye miguu yake namna *hiyo*. Alikuwa akienda, "Ooooooh." Akaanza kuja upande wangu, kwa kasi kadiri alivyoweza.

Nikasema, "Loo, Bwana Mungu, Damu ya Yesu Kristo inilinde na kitu hicho!"

Ndipo Wayne akaruka kitandani, akaangalia. Na kilikuwa hapa, kama kivuli kikubwa, kimezunguka, kisha kikaenda na kushuka nyuma ya kitanda. Wayne akachomoka kitandani, akaingia chumba kingine, mbio alivyoweza kukimbia. Kwa hiyo sisi ...

135 Nikamchukua Nellie na kumpeleka nyumbani. Kisha nikarudi, nami nisingeweza ...

Mama aliingia mle na kutikisa shuka na kila kitu. Hakukuwa na kitu katika kitanda hicho. Ilikuwa ni kitu gani? Pepo alimtoka. Kulitokea nini? Alisimama kwa muda kidogo. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara mbili — Mh.] Hivyo tu.

Usisimame, hata kidogo. Wakati Mungu anapoliingiza Neno Lake moyoni mwako, chukua tu Upanga huo na uanze kukata na kukata. Haleluya!

"Sina wakati wa kungojea kitu kingine. Nimevuka tu hivi punde, sina hata muda wa kuketi nipumzike."

136 Akasema, "Uchukue fimbo yangu na kuiweka juu ya mtoto. Na kama mtu ye yote akikuzungumzia, hata usimjibu.

Kama ibilisi akisema, 'Aisee, unajua unavyojisikia?' Hata usizungumze naye. Endelea tu kusonga mbele.

Ibilisi, mnajua, ibilisi anasema, "Lakini unajua nini? Unamjua, *Fulani na fulani*, walipompokea Roho Mtakatifu, unakumbuka wao—karibu warukwe na akili." Hata usizungumze naye. Endelea kusonga mbele. Hujui kuhusu *Fulani*.

137 Ni wewe na Mungu. Hiyo ni kweli. Mshikilie Mungu. Yeye huwatia mafuta watumishi Wake. Sina budi kuharakisha. Mungu huwatia mafuta watumishi Wake. Mnaona?

Sasa, yanilazimu niruke muhtasari mdogo hapa, lakini ningetaka kusema jambo hili. Hapa, sikilizeni sasa, kwa makini.

Bibi mdogo, sikiliza kwa makini sasa. [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.]

Hapa tunaona mbinu za Ibilisi. Tunafanyaje? Sasa, nina Maandiko mengi sana hapa, ya manabii na kadhalika, ambapo aliwajia, na watu mbalimbali katika Biblia, na kufanya jambo lile lile. Daima ni mbinu yake, ni kujaribu kuwafanya watu wasiliamini Neno la Mungu. Sikilizeni, enyi askari wa msalaba. Unapokosa kuamini Neno moja la Biblia iliyoandikwa ya Mungu, unapokonywa silaha.

138 Unaamini hilo, mpenzi? [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.]

Umepokonywa silaha. Unajisalimisha, yavuyavu wewei. Vaeni silaha zote za Mungu. Amina. Tuko vitani. Yale Mungu aliyosema ni kweli. "Kila neno la mwanadamu ni uongo." Mnaona? Lakini mara tu wewe —anakufanya kusikiliza jambo moja, hizo ndizo mbinu zake, umenyang'anywa silaha.

Hawa alipaswa kusikiliza mambo mangapi? Moja. Alipokonywa silaha papo hapo. Ibilisi alifanya nini? Aliingia ndani moja kwa moja kupitia akili zake hadi kwenye roho yake, na hapo akapotoshwa. Hiyo ni kweli? Alipotoshwa dakika ile ile aliponyang'anywa silaha, wakati alipolikataa Neno la Mungu. Vema. Hapa tunaona mbinu zake.

139 Askari wa Mungu wanaamriwa "Vaeni silaha zote za Mungu." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa, kama unataka kuandika Andiko hilo, linapatikana katika Waefeso 6:10 na 13. Mnaona? Tulilisoma muda mfupi uliopita. Ni somo letu. Vema. Angalia. "Vaeni silaha zote za Mungu." Hebu ... Je! Una muda wa dakika chache? ["Amina."] Hebu na turudi hapa kwa dakika moja. Hebu tuone tu silaha zote za Mungu ni nini. Vema. Hebu tuanzie kwenye aya ya 10. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa. Hebu na tupate silaha zote za Mungu. "*Hatimaye, ndugu zangu ...*" Sasa, ninajua ninaenda ... Nina ...

140 Ni dakika ishirini, sasa hivi, hadi saa kumi na mbili, ni kama tu. Si—sininii ... Sikutaka kuwafundisha muda mrefu leo, bali mimi—mimi huenda nisiwe na ujumbe mwingine zaidi hadi nitakapofanya baadhi ya ziara zangu kwa msimu wa kiangazi, mnaona.

141 Nanyi mnajua nini? Mnajua ni kwa nini ninafanya jambo hili? Nitawaambia. Hivi majuzi niliota ndoto. Sikuwa nikieleza jambo hilo, bali liko tu moyoni mwangu. Afadhali nifanye hivyo, baada ya Bwana kunipa tafsiri.

Niliota kwamba nilikuwa nikijiandaa kuvuka mto mkubwa, kwa ajili ya kazi ya umishenari. Na sasa, kwanza, nilikuwa huko juu pamoja na mke wangu ...

Na ni wangapi waliopata kumjua George Smith, Smith wa sekunde sita, hapa mjini? George Smith, mvulana wake yuko kwenye jeshi la polisi hapa. Yeye, maskini George, ni mlevi sasa. Lakini yeye alikuwa mmoja wa wapiganaji bora sana. Yeye ndiye aliyenipa mafunzo yangu, kabla hata hajaenda Y.M.C.A. na popote. Alikuwa akitufanyiza mazoezi. Naye alikuwa mwepesi, mwepesi sana. Yeye akiwa tu mwana ndondi wa uzito wa kati, wa ratili 145. Naye alinifundisha mimi. Naye alikuwa akisimama pale, naye angeweza kuchukua ngumi yake, namna *hiyo*, na kunipiga moja kwa moja tumboni, akaniinua ukutani, unaona, lakini, na hilo halinisumbui. Yeye alinifundisha tu, hakukuwa na kitu ila kufundishwa tu.

142 Halafu basi ni—niliota, hivi majuzi usiku, kwamba nilimwona Smith wa sekunde sita. Sasa, haikuwa ni ono. Ilikuwa ni ndoto. Nami nikamwona Smith wa sekunde sita, vijana wakija dhidi yake, katika kupigana mieleka. Naye, huyo mzee, karibu, loo, nadhani ... Nina umri wa miaka hamsini na miwili. Yeye ana umri wa miaka hamsini na minane, sitini. Hakukuwako na yeyote wa hao vijana angeweza kumgusa, kwa njia yo yote. Angewabana pamoja, namna hiyo, akawaangusha chini sakafuni na kuwashikilia kwa mkono wake.

Nikawaza, "Hilo ni jambo la ajabu." Nilifikiri mke wangu alikuwa pamoja nami, nikasema, "Hilo ni jambo la ajabu." Nikasema, "Unajua nini, Meda? Alikuwa mkufunzi wangu."

Akasema, "Na—nakumbuka jambo hilo, wewe ukiniambia habari zake."

Nikasema, "Naam, bwana. Kwa mafunzo yake mazuri, nilishinda mapambano kumi na tano ya kitaalamu, na nikaacha ninii—kazi hiyo; kuihubiri Injili."

143 Punde tu ikabadilika, na nilikuwa ninaanza kuvuka ma—maji. Lakini nilipokuwa ninakwenda, nilikuwa nikienda kwa motaboti. Nami nikaangalia kule ng'ambo, na hapo waliketi wawili kati ya ndugu zangu, wameketi mle katika mtumbwi, wakijitayarisha kwenda pamoja nami. Nikasema, "Hamwezi kufanya hivyo, wandugu. A-ha. Sina budi kwenda peke yangu."

Kisha yule baharia akaja akasema, "Hii hapa boti yako," mtumbwi mweupe kabisa, wa plastiki.

Nikasema, "La, aha. A-ha. Si huo."

Akasema, "Vema, unaweza kukimbia *huku* na *huku*, maili hamsini kwa saa."

Nikasema, "Lakini sina budi kuvuka upande *huo*." Mnaona?

"Vema," akasema, "nenda na *hao* jamaa."

Nikasema, "Wao si mabaharia. Hawajui vya kutosha kuhusu jambo hilo. Wana shauku. Hawawezi kuiendesha hiyo, Watakufa maji wote wawili nje huko. Hawawezi tu kufanya hivyo."

Basi akasema, "Wewe ni—unaweza kuamini..."

Nikasema, "Sikiliza, na—najua mengi zaidi kuhusu boti kuliko wanavyojua, na nisingejaribu kuiendesha kwa hicho—kifaa cha namna hiyo." Nikasema, "Inabidi kuchukua motaboti kuivuka hiyo." Nikasema, "Itahitaji kitu fulani kikubwa kuliko huo."

144 Na nikamwona akiangalia pande zote, kwa mmoja wa wale ndugu, akasema, "Je! nyinyi ni mabaharia?"

Hao ndugu wakasema, "Naam." Mnaona?

Nikasema, "Hilo ni kosa."

Na yule baharia akarudi. Akasema, "Nitakwambia la kufanya." Kasema, "Wanakupenda. Wanakuamini. Lakini," kasema, "kama ukijaribu kuvuka kwa motaboti, hao watajaribu kukufuata wewe katika mtumbwi ule. Wote wawili watakufa, mnaona." Kasema, "Hawawezi kukufuata."

Nami nikasema, "Vema, nifanye nini?"

Basi huyu baharia bandarini, akasema, "Rudi *kule* juu." Kasema, "Kuna ghala moja tu ndogo katika nchi hii yote, ghala moja ndogo. Basi weka tu akiba nyingi," kasema, "nao watakaa hapa. Wata—watakaa hapa uta—utakapokuwa umeondoka. Lakini," kasema, "itakubidi kuweka akiba."

Nami nilikuwa nikiagiza tu kila namna ya kabichi, na mboga kama muhogo, na figili, na kadhalika, nikizilundika mle ndani namna hiyo. Ndipo nikaamka.

Sikujua ilikuwa ni nini, bali ninajua sasa. Tunaweka tu akiba, enyi ndugu. Haya ni maisha ambayo inakubidi kutembea peke yako.

145 Leo, unakumbuka ile ndoto uliyoota wakati ule ulipokuja hapa kwa mara ya kwanza? [Ndugu Leo Mercier anasema "Amina." — Mh.] Kuhusu piramidi, na ulidhani ulingekuja mle ndani. Nikasema, "Leo, hakuna mtu anayefika hapa juu. Mungu hana budi kumweka mtu hapa juu. Ulipanda kila namna ya maumbile ambayo yanaweza kupandwa." Nikasema, "Huwezi kuja hapa, Leo. Mnaona? Rudi chini. Waambie tu watu ya kwamba linatoka kwa Mungu." Mnaona? Mnaona?

Ni kitu ambacho hu—huwezi ukakitegemea, hata ndugu zangu na dada, na kanisa langu na kila kitu, na hata makanisa mengine jinsi yalivyo mema, na ndugu zangu kila mahali.

146 Sasa, siwezi kujitenga na kanisa huko nje. Mtu fulani anasema, "Vema, kwa nini unakwenda huko na hao watu, hao watu wa Utatu, wote *hawa*, wale na wengine, wale wa Oneness, na Jina la Yesu, na yote

haya mambo mengine nje hapa. Kwa nini unachanganyika nao, kwa vyo vyote?” Wao ni wangu. Haidhuru wamefanya nini, wao ni wangu. Hao ni mimbara yangu.

Wakati Israeli walipotenda uovu mbaya sana, mpaka hata Mungu akamwambia Musa, kasema, “Jitenge; Nitaanza kabila—kabila jipya nawe,”

Musa alijitupa njiani akasema, “Kabla ya Wewe kuwaangamiza, niangamize mimi.”

Haidhuru walikuwa wamefanya nini, hao ndio ambao nimetumwa kwao. Yeye hutuma Nuru, si kuangaza palipo na Nuru. Mahali palipo na giza, hapo ndipo mahali pa Nuru. Inakubidi usimame pamoja nao haidhuru nini. Huna budi kusimama pamoja nao, haidhuru, huna budi, katika makosa yao.

147 Israeli walikuwa amekosea kupindukia. Walikosea sana, hata Mungu akawatoa. Lakini, Musa, Siku zote nimestaajabu jinsi hilo lilivyofanyika. Mnaona?

Mnaona, sote tumekosea. Yeye alitupigania sisi sote, tulipokuwa katika makosa yetu.

Haidhuru wao wamekosea vipi, hebu tusijitenge na ushirika wala kujitenga na chochote. Maadamu tunaweza kumvuta mtu, hebu na twende na “busara kama nyoka, wapole kama huwa” mnaona, na tujaribu kumvuta kila mtu tuwezaye.

148 Sasa, hiki ndicho ninachosema asubuhi ya leo, ni kuhifadhi Chakula. Kuhifadhi Chakula, kusudi upate kitu cha kula, ili kwamba uwe na kitu cha kula. Kiwekeni Hicho kwenye kanda zenu. Mkaziweke katika chumba chenye baridi. Pengine wakati mrefu baada ya kuondoka kwangu, mngali mtakumbuka mambo haya kuwa ni kweli. Ketini chumbani mwenu mkazisikize. Mnaona? Na hiki ni Chakula, kinachohifadhiwa, katika ghala. Sijui safari yenyewe ni ya wapi. Bali hata iwe ya wapi, Yeye anajua ambako anaongoza, mimi sijui. Ninafuata tu.

149 Sasa, yeye alisema nini hapa sasa? Sikilizeni kwa makini.

*Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uweza wa nguvu zake.*

*... Iweni hodari ... katika uweza wa nguvu Zake.*

*Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani.*

*Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, ...*

Kupigana risasi na kukatana kwa visu, mnaona, si jambo hilo

*...bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa...giza la dunia hii,...*

150 “Wakuu wa giza.” Ni nani anayeutawala ulimwengu? Ibilisi. Hakika. Ni nani ambaye anaendesha mambo yote haya, mambo yote haya maovu, yanayotendeka mahali pote hapa, na hizi serikali, na kadhalika? Yote ni ibilisi. Biblia ilisema hivyo. Ibilisi hutawala Marekani. Ibilisi hutawala Ujerumani. Ibilisi hutawala kila taifa ulimwenguni. Ninalifikia, katika dakika chache tu, nasi tutaona kama anafanya hivyo, ama la. Kama ... Kila ufalme uliowahi kuwako na utakaokuwako, mpaka Mungu atakaposimamisha ufalme Wake, unatawaliwa na Ibilisi.

Simaanishi kila mtu ndani yake ni ibilisi, sasa. Kuna watu wacha Mungu katika—katika ofisi za serikali.

151 Kutakuwako na mmoja hapa katika siku chache usiku, papa hapa, kuonesha picha hapa pamoja na Ndugu Arganbright, hapa mahali hapa. Yeye amekuwa balozi kwa maraisi watano mbalimbali, Ndugu Rowe. Naye ni ninii ... Atakuwa hapa, nafikiri ni katika juma la pili mwezi wa Aprili. Ndugu Neville atatangaza hilo. Naye ni mtu mzuri sana.

Yeye alisema angeweza kunena katika lugha nane mbalimbali, ninaamini. Lakini wakati alipompokea Roho Mtakatifu, hakuwa na lugha yo yote aliyoweza kuzungumza na Bwana, kwa hiyo Bwana alimpa moja tu, akasema, kwa hiyo akazungumza Naye na huyo. Alimpa mpya, ambayo hakuwahi hakufanyia mazoezi. Vema.

*...juu ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*

*Kwa sababu hiyo...*

Sasa, sikilizeni, enyi askari wote sasa, kabla tu hatujaanza mstari wa maombi.

*...twaeni zenu ... zenu (z-o-t-e)...zote (siyo sehemu yake tu)...silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, ...*

Hiyo ndiyo siku tunayoishi.

*... na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.*

*Simama ...*

Amina. Mnalipata hilo? Unaona, mpenzi? [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] Unapofanya yote unayoweza kufanya, kusimama, basi simama. Usisogee.

*Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni...*

Sikilizeni jambo hili. Sikilizeni hapa, hili ni nini. "Viunoni" Yaani sehemu yako ya katikati, hapa, mnaona?

*... mmejifunga kweli, ...*

Kweli ni nini? Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. "Neno Lako ni Kweli." Vema.

*...na kuvaa dirii ya haki kifuni,...*

Hiyo ni kusema, "Fanya yaliyo haki." Una Neno la Mungu ndani yako, ukitenda yaliyo haki. "Dirii ya haki."

*Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;*

Unaenda po pote, mahali po pote, wakati wo wote; miguu imefungiwa Injili. Mnaona? Na tazama:

*Zaidi ya yote, zaidi ya yote hayo, itwaeni ngao ya imani, ...*

Hiyo ndiyo inayoiangusha mishale, mnaona, "ngao ya imani."

*... ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote ya yule mwovu.*

*Ipokeeni chapeo ya wokovu,...*

Hiyo ni nafsi ... Akili—akili, humu ndani, kichwa; hukifunika kichwa.

*... na—na upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu:*

152 Utaifanyaje chapeo hii, inafanya nini? Ni kinga. Chapeo imetengenezwa kwa nini? Shaba. Shaba hata haiwezi kutiwa matiko; ni ngumu, ngumu kuliko chuma. Kofia ya shaba, (nini?) Wokovu, ujuzi wa jambo hili, "Kwamba kuponywa kwangu hutoka kwa Mungu. Wokovu wangu unatoka kwa Mungu. Ujuzi wangu unaambatana na Neno Lake, si wazo la kanisa; Neno!" Amina. Haya basi. Kufunikwa, kwa kinga, chapeo ya wokovu, ukombozi. Chukua hiyo, kisha uendelee mbele. Loo, sasa, Sasa hilo ndilo tunalopaswa kutenda. Jeshi la Shetani ...

153 Sasa angalia, sasa, sisi ... Yanibidi niharakisha, bali ya—yanibidi niingize hili ndani.

Jeshi la Shetani huleta magonjwa. Hivyo ndivyo Shetani alivyo, yeye ni mharibifu. Shetani, ufalme wote wa Shetani, ni maradhi, mauti, na huzuni, na mahangaiko ya moyo, na wasiwasi, vyote juu ya Shetani.

Mungu ni Uzima, imani, furaha, amani, hapa. Mnaona?

Sasa, hizo ndizo zile nguvu kuu mbili zinazopambana sasa hivi. Zinapigana. Zinapigana papa hapa katika jengo hili sasa hivi. Zinapigana, na wewe siku, baada ya siku, kila nguvu.

Shetani, akikufuatilia, yule Goliathi mkubwa, mno, wa kifalme, na wa kikasisi, akijaribu kukufadhaisha kupita kiasi. Yeye yuko moja kwa moja, lakini Mungu ...

Umeimarishwa, amina, kwa Injili, kwa Neno la Kweli viunoni mwako. Utukufu! Mhubiri, jambo ndilo hilo. chapeo ya wokovu; ngao ya imani, na Upanga ukitikiswa mkononi mwako! "Shetani, naja kupambana nawe. Unanijia kwa jina la sayansi. Unanijia kwa jina la—la utamaduni. Unanijia kwa jina la madhehebu. Unanijia kwa jina la hili, lile, au lile jingine. Lakini ninakujia katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli. Ninakujia. Hima!" Hata kifo chenye hakiwezi kusimama pale. Toboa tundu ndani yake. Hiyo ni kweli.

154 Jeshi la Shetani huleta maradhi, na jeshi la Mungu limeagizwa kuyaondoa. Amina. Haya basi. Kila wakati Shetani anapokutupia, cho chote, jeshi la Mungu lapaswa kumtoa. Amina. Mtoe!

Hiyo ndiyo mbinu hasa ambayo Mungu alitumia. Shetani alitumia jeshi la uharibifu kwa kutokuamini Neno la Mungu, na kujitengeneza ufalme bora kuliko aliokuwa nao Mikaeli, ndipo Mungu akamtupa nje.

Njia ya Mungu, ni, kutupilia mbali uovu. Kutupilia mbali hoja. Kutupilia mbali ushirikina. Kutupilia mbali hofu. Kutupilia mbali magonjwa. Tupilia mbali dhambi. Amina. Uko juu yake, umefufuka katika Kristo Yesu, umeketi katika ulimwengu wa Roho, huku kila pepo akiwa chini ya mguu wako. Kama akianza kutokeza



kichwa chake hapo, nini ...

155 Unajua, umekufa. Uhai wako umefichwa. Kitu gani kimekufa? Umekufa kwa hisi zako Umekufa kwa dhamiri yako. Mapenzi yako ya kibinadamu yangesema, "Naam, nadhani mimi ..." Umekufa kwa hoja zako. Umekufa kwa mambo yote hayo, Nawe umezikwa katika Jina la Yesu Kristo; na kufufuka pamoja Naye. Na po pote alipo Yeye, wewe nawe upo hapo pia.

156 Kulitukia nini wakati wao, mmoja wa hao wanaoshuku alipofika Mbinguni? Mungu alimtupa nje. Na Yeye aliwaambia nini askari waliofufuliwa katika Kristo? "Ibilisi ajapo, mpigeni teke. Mtupeni nje." Wakati Yesu alipolifundisha jeshi Lake, na kuwaagiza hata miisho ya dunia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumwa. Na ishara hizi zitafuatana na waaminio, askari Wangu. Kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watahika nyoka, au wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia.

"Nimesulubiwa pamoja Naye, hata hivyo ninaishi; si mimi niishiye, bali Yeye aishiye ndani yangu." Neno likitangulia, mbele, Mungu akitengeneza njia, kwa upanga Wake wenye makali kuwili.

157 Halafu, si ajabu, wakati Grant alipouteka Richmond, na maskini yule mwanamke mdogo wa kusini akamwona Grant akija, alipata upako. Naye akasema:

Macho yangu yameona utukufu wa kuja kwa Bwana;  
Yeye anakanyaga palipowekwa mavuno ya zabibu kwa hasira;  
Yeye aliachilia umeme wa kutisha kwa upanga Wake mwepesi wa kutisha;  
Majeshi yake yanasonga mbele.

158 Amina. Grant aliutekaje Richmond? Mara tu alipolifikia. Amina. Hivyo ndivyo alivyouteka Richmond.

Hivyo ndivyo askari wa Mungu wanavyoshinda dhambi, maradhi; mara wanapoyafikia. Amina. Hivyo ndivyo wanavyoshinda mashaka yao, na hofu, na kadhalika. Wakati mmoja anapoinuka, wanamkata. "Ondoka njiani!" Loo, jamani! Ndivyo ilivyo. Mungu aliwatoa, kama Yeye alivyofanya Mbinguni. Kapteni wetu Mkuu maarufu alituonesha jinsi ilivyotendeka. Amina.

159 Roy Roberson, Ndugu Funk, wengi wenu ninyi wanajeshi wa siku nyingi hapa, mwajua kapteni halisi ni nini.

Siku moja nilipokuwa mdogo tu...Idara ya Zimamoto ya Jeffersonville chini hapa. Nyumba ya Pfau ilishika moto. Na hii hapa Idara ya zimamoto ya Jeffersonville wakisimama chini kule, na kapteni akitembea huku na huko, akasema, "Rusha maji kidogo kule juu." "Sp-sp-sp-sp-sp," kama bomba dogo nje hapa. Hapa kukaja Clarksville, "Rusha maji kidogo *hapa*." Rusha maji kidogo kule juu." Jengo la Pfau likateketea.

160 Wakapiga simu Louisville. Hawa hapa wanakuja watu waliofunzwa. Loo, jinsi hivyo ving'ora vilivyolia kila mahali hapo!

Na hawa hapa makapteni wakuu hapa, wa idara hizi za zimamoto wanasema, "Rusha maji kidogo juu hapa. Rusha maji kidogo chini *hapa*" Watu wasiofunzwa.

Ndugu, mara tu injini ile iliposimama, nani aliyekuwa juu kabisa ya ngazi? Kapteni. Wakati ngazi hiyo ilipopandishwa juu, alikwea pamoja nayo. Wakati alipogonga dirisha, hakuwa amefika kwenye dirisha bado. Alikamata shoka lake na akalitupa kupitia kwenye dirisha, akasema, "Njoni, enyi vijana." Na moto ulikuwa umezimika, katika dakika chache. Kapteni!

Si kapteni, aseme, "Mwagilia maji kidogo *hapa*. Jaribu kidogo *hapa*."

Lakini, "Njoni, enyi vijana!" Amina. Aliongoza njia. Yeye alituonesha jinsi linavyofanywa.

Nikawazia, "Hiyo idara ya zimamoto iliyofunzwa vizuri, waliuzima moto huo katika dakika chache." Kwa nini? Walikuwa na kapteni pale aliyejua alichokuwa akifanya.

161 Ndugu, nena kuhusu theolojia yako yote unayotaka. Madhehebu yenu yaliyoundwa na binadamu, mashirika yenu, cheza nayo.

Nina Kapteni Mkuu aliyeniambia jinsi ya kufanya jambo hilo.

Sema, "Naam, kama naweza kusikia harufu yake, kuihisi." Loo, upuuzi!

Hivi ndivyo yule Kapteni Mkuu alivyosema inafanywa, katika Luka sura ya 4. Sina wakati wa kulisoma.

Soma jambo hilo, wewe mwenyewe. Vema. Luka sura ya 4, kuanzia kifungu cha kwanza.

Hakusema kamwe, "Sasa, nitawaambia. Hebu nendeni *huku* mkaunde madhehebu makubwa. Wekeni wazee, na mashemasi, na, au wekeni makadinali na maaskofu na wekeni *hili*." Yeye hakusema jambo hilo kamwe.

Wakati Shetani alipokutana Naye, alisema, "Sasa Wewe una njaa. Geuza mawe haya yawe mkate."

Yeye alisema, "Imeandikwa ..."

Alisema, "Juu huku, tutakuchukua juu huku na kukuonesha jambo fulani."

"Lakini imeandikwa ..."

"Nitafanya jambo *hili*, kama Wewe ukilifanya."

"Imeandikwa ..."

162 Hivyo ndivyo yule Kapteni Mkuu alivyosema linatendwa. Linatendwaje, Dada? "Imeandikwa, "Ukiweka mikono yako juu ya wagonjwa, watapata afya." "Imeandikwa, 'Katika Jina Langu watatoa pepo.'" Amina. Ni kitu gani? "Imeandikwa!" Hiyo ndiyo amri ya Kapteni. "Imeandikwa, 'Kila asikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.' Imeandikwa! Imeandikwa! Imeandikwa!" Hayo ndiyo —hayo ndiyo maagizo. Huyu ndiye yule askari. Hiyo ndiyo njia. Hiyo ndiyo mizinga tunayosogeza mbele.

163 Alifanya nini? Alienda moja kwa moja pale, kwa Goliathi. Yeye alionyesha ninii ... Daudi alioneshaje jeshi jinsi ilivyotendeka? Aliwaoneshaje Israeli jinsi ilivyofanywa? Daudi maana yake ni "mpendwa, mwokozi." Mnaona? Daudi alifanyaje jambo hilo? Alisema, "Hivi ndivyo inavyofanyika. Litumaini Neno la Bwana."

Ndipo Goliathi akaja pale, akasema, "Unajua nini? Nitakuokota kwa ncha ya mkuki huu, nitakulisha ndege wewe."

Akasema, "Unanijia kama dhehebu. Unanijia kama mwanasayansi wa kisasa. Unanijia na upanga wako mkubwa mno wa futi kumi na nne. Unanijia na chapeo ya shaba, na kipande cha ngao ambacho hata siwezi kukiinua toka ardhini. Unanijia nami kama shujaa aliyefunzwa. Unanijia na Ph.D, na L.L.D. na L.D. maradufu. Unanijia mimi katika mambo haya yote. Bali mimi naja katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli, na leo nitakikata kichwa chako toka kwenye mabega yako." Amina. Maskini kijitu hicho kikijitokeza pale kulikabili hilo pandikizi la mtu, bali alijua mahali alipokuwa amesimama.

Israeli, wakitetemeka kule nyuma, "Loo, maskini jamaa mdogo."

Goliathi akasema, "Nitakuonyesha ni nani nitakayefanya." Naye huyu hapa anakuja.

164 Alikuwa na I-m-a-n-i, mnaona, k-a-t-i-k-a J-e-s-u-s, miamba mitano, mawe matano. Kijiwe kimoja ndani hapo cha kuanzia. Akikizungusha pande zote namna hiyo, Roho Mtakatifu akalishika jiwe hilo, nalo likaenda. Goliathi akaanguka chini. Hivyo ndivyo inavyofanyika.

Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, yale aliyosema. "Sasa, kama ninyi ndugu mnaenda katika shamba la huduma, kama tunataka kujua jinsi ya kuwashinda hawa pepo, nitawaonesha namna inavyofanywa."

165 Shetani akasema, "Nitakutana nawe." Goliathi, "Nitakuonesha kile ninachoweza kufanya. Una njaa. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, nitakupa changamoto. Unasema Wewe ni Mwana wa Mungu. Nitakupa changamoto. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate. Kula; Una njaa. Na kama Wewe ni Mwana wa Mungu, una nguvu za kufanya jambo hilo."

Yeye alisema, "Lakini imeandikwa, sasa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu.'" Loo, hivyo ndivyo Amiri Jeshi Mkuu alivyofanya jambo hilo.

Akamchukua akamweka juu ya kinara cha hekalu. Yeye alisema, "Ukijitupa chini," kasema, "Unajua pia imeandikwa pia ..."

Kasema, "Naam." Kasema, "Imeandikwa, tena, 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.'" Mnaona kile alichojiita Mwenyewe? "Bwana Mungu wako." A-ha. "Usimjaribu Bwana Mungu wako, 'imeandikwa, tena, namna hiyo.'" Mnaona? Loo, jamani!

166 Yeye alifanya nini? Alimshinda, kwa Neno la Mungu. Mbinu ya Ibilisi ni kukufanya usiliamini Neno la Mungu. Naye Kapteni Mkuu akasema, "Chukua Neno la Mungu na ulitende. Katika Jina Langu watatoa pepo."

167 Loo, Shetani, kapteni wao mkuu, loo, unajua, baadhi ya haya madhehebu yanajaribu kukufanya uamini ana ukwato panda, mnajua, na mkia uliogawanyika, na upuzi huo wote. Msiamini jambo hilo. Yeye hayuko hivyo. La, bwana, ndugu. Yeye ni mjanja sana. Msiamini ana hayo. Wanafanya hivyo tu kukuogopesha. Huyu si Ibilisi. Ibilisi kwanza hana ukwato, nalitilia jambo hilo shaka sana. Yeye ni roho tu.

Ibilisi ni roho. Yeye hana kwato panda na vitu hivyo jinsi wanavyojaribu kumwazia. La, la.

168 Lakini, yeye ni mwenye hekima. Ndugu, yeye ni mtu mwenye busara sana, mtu aliyeelimika kwelikweli, sikuzote imekuwa hivyo, katika hekima ya kidunia. Loo, naam. Yeye ni mrembo. Ameliunda jeshi lake kwa hekima ya kidunia, hadi, Ndugu, usijaribu ku—usijaribu kunena maneno yako. Afadhali ujue unachozungumzia unapokutana na mmoja wa hawa jamaa, wakisema, "Siku za miujiza zimepita." Sasa, yeye hana—hana ukwato panda. Yeye ni, loo, yeye—yeye—yeye ametoka moja kwa moja seminari. Yeye ameadibishwa, ndugu. Ninamaanisha, yeye ni mwerevu, Ph.D., L.L.D., Q.U.S.T., na mengine yote. Mnaona? Wote mle ndani, yeye ni mwerevu tu awezavyo kuwa. Mwenye hekima, hakika, yeye ni nyoka, mjanja kuliko wote. Nywele zimechanuliwa vilivyo, ndugu, namaanisha amevaa, na hakuna hata kunjio katika koti. Ni mwerevu, ana hekima na ni mwerevu kwelikweli. Hiyo ni kweli.

Usimchezee isipokuwa uwe unajua unachozungumzia. Hiyo ni kweli. Loo, bali tunajua mbinu zake za kale—mbinu zake za kale. Tunajua kile anachojaribu kufanya: kutufanya tusiamini Neno la Mungu.

Naye hana kwato panda. La, la, la. Sasa, tunaona kwamba kama hana kwato panda, basi lazima awe ni kitu kingine. Yeye ni mjanja sana. Yeye ni hekima, amelimika, ameunda madhehebu. Ndugu, ameliweka jeshi lake hivyo.

169 Angalia, wakati mmoja, huko Uswisi. Siwezi tu kupata mahali pa kukomea, jamani. Kuna ninii—ninii ... Kule Uswisi, kukaja lile jeshi la Kijerumani, ninii- ... pamoja na wageni wakiingia. Mbona, lilionekana kama ukuta wa matofali; Kila mtu amefunzwa, kila mkuki umewekwa *hivi*, futi nane au kumi mbele. Nao wakawajia maskini Waswisi wachache juu kule, walikuwa na nini? Walikuwa wana silaha za—na visu vya miundu yao, fimbo na mawe, na hao hapo wakiwa wamesimama. Wangelikabiliana nao. Huko ng'ambo ya kilima kulikuweco makazi yao. Hapa jeshi la Waswisi lilitoka kwenda kupambana nao. Hawakuwa wamewatendea kitu cho chote. Walikuja tu wakaiteka nchi yao.

170 Mtoto huyu amefanya nini ulimwenguni, mtoto mdogo tu? Shetani, huyo ndiye ambaye angechukua uhai wake kama angeweza. Hakika. Huyu hapo; kabla ya wakati wake. Mnaona?

Waswisi hawajafanya lolote. Walikuwa watu wazuri. Walikuwa wakijaribu kulinda makazi yao, bali walisimama nje huko kuyalinda. Baada ya muda kidogo, akatokea mtu mmoja jina lake Arnold von Winkelried. Hili hapa jeshi linakuja. Wote walikuwa wamezungukwa. Kasema, "Tufanyeje?"

Kila mahali, bahari tu za watu, waliofunzwa vizuri. Hivyo ndivyo Shetani anavyofanya. Wamefunzwa vizuri, mkuki wake umeelekezwa mbele tu, kila mtu anapiga hatua kwa utaratibu, moja, mbili, moja, mbili, wakilikaribia tu hili jeshi dogo. Wali—waliendelea tu kutembea, hilo tu ndilo lililowabidi kutenda huku wakiwaokota, kila mmoja, kwa mapanga yao. Ile mikuki ikiwachoma moja kwa moja miilini mwao. Huo ungekuwa ndio mwisho wa jeshi la Kiswisi. Hamna jambo lingine. Huko juu kilimani kulikuwa na makazi yao pamoja na wapenzi wao. Na hao wanawake wangetendwa jeuri, na kunajisiwa, na binti zao wadogo, na watoto kuuawa na nyumba zao kuchomwa moto, na kila kitu, chakula kuchukuliwa, mifugo na kadhalika, kuchukuliwa. Hao hapo.

171 Ni kitu gani kilichotukia? Uvuvio ulimgusa mmoja kwa jina la Arnold von Winkelried. Akasema, "Enyi watu wa Uswisi, leo hii nitakufa kwa ajili ya Uswisi." Amina. "Leo hii nitakufa kwa ajili ya Uswisi."

Wakasema, "Utafanya nini?"

Akasema, "Nifuateni mimi mkapigane na yote mliyo nayo." Akasimama juu kule; akatupa mkuki wake chini, fimbo yake ndogo aliyokuwa nayo mkononi mwake hivyo, namna *hiyo*. Naye akapiga kelele, huku ameinua mikono yake juu, hivyo, na akakimbia kulielekea, akipiga ukelele, "Wekeni njia kwa ajili uhuru!" Katimua mbio haraka alivyoweza moja kwa moja kwenye lile jeshi. Naye, alipofanya hivyo, akanyakua kila mmoja wa mikuki aliyoweza, na kuichomeka moja kwa moja katika kifua chake namna *hiyo*, akafa.

172 Yeye aliwaambia, kabla hajaondoka. kasema, "Kuna maskini nyumba moja ndogo juu kule, mke na watoto wachanga wachache, ninaacha makazi madogo ndiyo kwanza niyanunue." Kisha akasema, "Ni—ninawapenda, lakini leo, nitakufa kwa ajili ya Uswisi." Yeye alitoa ninii yangu ... Yeye alisema, "Natoa maisha yangu kuliokoa taifa." Na huyo alikuwa shujaa. Hawajapigana vita tangu zamani hizo. Hilo, hilo liliimaliza.

Liliangamiza kabisa jeshi lile, kwa ushujaa ule uliooneshwa, mpaka hapakuwa na ... Lile—lile jeshi lilichanganyikiwa sana. Waswisi waliwavingirishia mawe, na kuwafukuza kutoka nchini, na kamwe hawajarudi tangu wakati huo. Hiyo imekuwa mamia ya miaka iliyopita. Mnaona? Kwa nini? Hilo lilikuwa tendo kubwa.

173 Lakini, loo, ndugu, siku moja wakati ujinga, ushirikina, shaka, kuhangaika, na woga viliwakandamiza watu wa Mungu pembeni. Kulikuwa na Mtu mmoja jina Lake Yesu Kristo aliyesema, "Leo hii nitakufa kwa ajili ya watu." Hiyo ni kweli.

Aliliambia nini jeshi lake? “Nifuateni Mimi mkapigane na kila kitu mlichio nacho. Kama una rungu, shambulia kwa rungu. Usiogofo. Kama una fimbo, shambulia kwa fimbo. Kama una jiwe, shambulia kwa jiwe, cho chote ulicho nacho.”

Hivyo ndivyo Kapteni wetu Mkuu asemavyo leo. “Nimelichukua Neno la Mungu, na kumshinda ibilisi katika nguvu zake.” Alimkatakata vipandevipande, amina, kwa lile Neno. Sasa, lo lote ulilo nalo, kama unalo Neno moja tu, “Bwana Mungu Mungu wako, ndiye akuponyaye,” mkatekate. Fuata. Amina. Mfuateni Kapteni wetu. Naam, bwana. Yeye alimkata.

174 Shetani, na milki zake kubwa, na nzuri, na uzuri zaidi, na kila kitu, vyote vya kisasa. Havituhusu sisi. Hiyo ni kweli. Yeye yungali mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu. Naam, bwana. Yesu alisema ya kwamba watoto wa ulimwengu huu walikuwa na hekima kuliko watoto wa Ufalme wa Mungu.

Sasa, haya mapambano mawili makuu. Tutaenda ... Sina budi ... sina budi kufunga. Mapambano haya mawili yanakabiliiana sasa hivi. Hivi sasa ndiyo saa ambapo magonjwa na kadhalika vimeukumba ulimwengu, mpaka sayansi ya utabibu imeduwaa, na kila kitu kimeduwaa. Hakuna kitu, na—na tutaninii tu ... Na jeshi, lile jeshi dogo la Mungu, linaungwa mkono pembeni na kila kitu. Ndugu, ni wakati wa Arnold von Winkelried mwingine. Ni wakati, wakati wa mtu mwingine wa Mungu kusimama. Ni wakati wa Eliya kutokea. Ni wakati wa jambo fulani kutukia.

175 Jeshi la Mungu, funga nia yako. Usisimame kwa dakika moja, kuwazia juu ya jambo lolote ambalo Ibilisi anakupa kwa hisi zako. Lakini kumbuka, Neno la Mungu haliwezi kushindwa kamwe.

Majeshi haya mawili makuu! Wakati adui anapokuja kama mafuriko, kama anavyokuja leo, Mungu alisema angefanya nini? “Roho wa Mungu angeinua kiwango dhidi yake.” Je! Wewe ni mmoja wao? Naam, bwana.

176 Tunafundishwa katika Yakobo 4:7 ... Sina wakati wa kulisoma. Yakobo 4:7, ya kwamba, “Mpingeni Ibilisi, naye,” hatatembea tu akienda zake, bali” atakimbia.” “Mpingeni Ibilisi.” Unampingaje ibilisi? Namna ile Kapteni wetu Mkuu alivyotuambia kufanya jambo hilo. Chukua Neno la Mungu. Hivyo ndivyo unavyompinga ibilisi, ni kwa Neno la Mungu. Kapteni Mkuu alituambia namna tu ilivyotendwa. Vema.

177 Sasa, katika kufunga, ninataka kusema jambo hili. Yule ibilisi mzee, sasa, unafikiri yeye ni mkali. Mnafikiri atamshambulia mtoto? Yeye atashambulia chochote. Alimshambulia Yesu Kristo. Yeye alimjia, akiwa na mashambulio mabaya matatu. Je! Ulijua jambo hilo? Shetani hakushambulia mara moja tu. Atakushambulia kwa ugonjwa, halafu hapa atarudi akushambulia, akisema, “Siku za miujiza zimepita. Hukuponywa. Hakuna kitu kama hicho.” Unajua hiyo ni kweli?

Alimshambulia Yesu mara tatu. Mashambulizi matatu makali, alimshambulia Yesu, pamoja na kutokuamini kwake Neno la Mungu. Yesu alikuwa Neno. Hakika, hakuamini. “Ikiwa Wewe ... Ikiwa Wewe ...” Huyu hapa anakuja, mashambulio makali, kama wakati mwingine adui anavyofanya. Hawa hapa wanakuja, kasema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, nioneshe muujiza. Hebu nione ukifanywa.” Ndugu, mashambulio matatu makali aliyolingia nayo, “Ikiwa wewe ... Ikiwa wewe ...”

178 Sasa, Yesu alifanya nini? Yesu alikuwa Neno la Mungu. Yeye alikuwa Neno. Alilishambulia Neno. Utukufu! Ni—ninapata tu ... ninajisikia vizuri, kuhubiri sasa, kwa kweli mimi ni. Hiyo ni kweli. Yesu ni Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akakaa, akafanyika mwili, akakaa ...” Yesu alikuwa Neno. Yeye alifanya nini? Yeye alimkatakata vipandevipande. Loo, jamani! Nitamaliza. Yesu alifanya nini? Yeye alikuwa Neno. Kwa hiyo, kwa Neno, Yeye alimkata Shetani kwenye mashambulio yake makali. Yeye alimrukia pale kama kikosi cha askari, au kikosi cha askari hodari wanaoshambulia ghafla au kitu kama hicho, akamrukia Yesu, lile Neno, namna hiyo. Naye Yesu akalichukua Neno hilo, na kumkata vipandevipande. Haleluya! Hakika, alimkata vipandevipande, akamshinda kwa Neno.

179 Unaona shambulio lake? Angalia, sikiliza kwa makini, ninapofunga. Shambulio lake ni nini? Kutokuamini Neno la Mungu, hilo ndilo shambulio lake. Hapo, unaweza kuona vita vikuu sana vilivyopata kupiganwa? Kuna nguvu mbili tu; Shetani na Mungu. Na silaha ya Shetani ni ipi dhidi yako? Ni kujaribu kukufanya usiamini Silaha yako. Yeye anakunyang'anya silaha. Hebu—hebu na tusikilize kimya kabisa sasa. Sikilizeni. Kama unaweza kukufanya usiamini Silaha yako ni sawa, akikufanya kuamini kwamba Silaha yako haina nguvu vya kutosha, amekunyang'anya silaha.

Loo, Ndugu Neville, natumaini hutaacha kamwe kuamini jambo hilo. [Ndugu Neville anasema, “Natumaini na siombe.” — Mh.]

Angalia. Yeye anakunyang'anya silaha wakati anapokufanya usiamini hiyo Silaha. Unapoweka Hilo chini, hilo linamaliza vita vyako. Umekwisha. Shikilia Silaha hiyo. Usiliweke chini. Tunaona kutokuamini kwake. Hebu ...

Jambo moja zaidi ninalotaka kusema sasa, katika dakika moja.

180 Urusi. Ninataka kusema jambo hili kwa manufaa ya mashujaa, na kadhalika, hapa, nanyi wanafunzi wa Biblia. Ni nini mnachozozana na kupiga makelele kuhusu Urusi? A-ha! Hamnisikii mimi nikiwaambia mjenge ngome za kujikinga na makombora, sivyo? Mbona hizi fujo kuhusu Urusi? Urusi si kitu. Hawatahinda vita vyo vyote. Hawatautwaa ulimwengu wo wote. Ukomunisti hautauteka ulimwengu wo wote. Watu wana nini? Neno la Mungu linaweza kushindwa?

Sikilizeni, hili kwenye kanda sasa. Kwa ulimwengu, ninazungumza, ama po pote kanda hizi zinapoweza kwenda. Na kwenu ninyi watu hapa, haidhuru lolote litakalonipata, aminini jambo hili.

Urusi, ukomunisti hauteki cho chote! Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Urumi itauteka ulimwengu.

181 Hebu na tuchukue ono la Danieli. Hilo ni Neno la Mungu. "Wewe, Ee Danieli ..." "Wewe, Ee Mfalme Nebukadreza, ni kichwa hiki cha dhahabu," Babeli. "Ufalme mwingine utakufuatia, ambao ni fedha" unaona, ambao ni wa Wamedi na Waajemi. Mwingine ni Uyunani, Alexander Mkuu. Halafu, akaingia, Rumi. Wala hakuna kitu kilichosemwa juu ya ukomunisti. Rumi iliuteka ulimwengu.

Yesu Kristo alizaliwa katika ufalme wa Kirumi, na kuteswa, mara Yake ya kwanza kuja hapa, na ufalme wa Kirumi. Na kwenye kuja Kwake mara ya pili, Akija sasa, Ujumbe Wake unateswa na madhehebu ya Kirumi, ambayo ni mama wa hao wote. Na wakati atakaporudi, atarudi kuufutilia mbali ufalme huo wa Kirumi, ambao Wayahudi daima wamemtazamia kuja na kuufutilia mbali ufalme wa Kirumi.

Utawala wa Kikatoliki pamoja na madhehebu yote ulimwenguni, sasa hivi wakikusanyika pamoja kama madhehebu, muungano wa makanisa wakijipanga pamoja. Si Urusi. Ni Rumi. BWANA ASEMA HIVI. Naam. Nioneshe Andiko ambapo ukomunisti, ama cho chote kingine mbali na Rumi, kitatawala.

182 Je! Wamedi na Waajemi walimfuata Nebukadreza? Hakika. Je! Uyunani uliwafuata? Naam. Je! Rumi iliutwaa tokea hapo? Je! ilivunjika katika milki kumi za Kituruki kama tu tulizo nazo leo? Je ...

Eisenhower, ambalo humaanisha "chuma." Khrushchev humaanisha ni "udongo." Je! hawakufanya mkutano wao papa hapa? Na Khrushchev akavua kiatu chake. [Ndugu Branham anagonga mimbara — Mh.] Kulifanya jambo dhahiri, wazi sana, akapigapiga nacho dawati, namna hiyo, kuwaonyesha watu. [Ndugu Branham anagonga mimbara.]

183 Vema, watu wana shida gani leo? Imani imekwenda wapi? Mbona, hivi huamini Neno la Mungu ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na kitu hicho hakiko hapa. Kuna nini kwa wahubiri siku hizi? "Ukomunisti!" Kila mhubiri yuko hapa nje akijaribu kupigana na ukomunisti. Ukomunisti, hakuna kitu!

Kitu hicho, ibilisi anakipenyeza moja kwa moja chini ya pua zenu nanyi humjui; ni Urumi, umadhehebu. Na Rumi ni mama wa madhehebu. Biblia ilisema, "Yeye alikuwa ni kahaba, na binti zake walikuwa makahaba," dhidi ya Mungu, dhidi ya Neno Lake.

Askari, chukueni Neno. Malaika wa rehema, kaeni na Neno hilo. Nitaangamia siku moja, bali Neno hili haliwezi kuangamia. Nanyi vijana, kama halitatendeka katika kizazi changu, mtaona. Hilo hapo jambo.

184 Mlisikia habari asubuhi ya leo? Bibi Kennedy akienda, akimwona papa, na yale papa aliyosema. Mnaona, dini zote za ulimwengu! Loo! Vema, labda tutapata mengi zaidi ya hayo, Jumapili ijayo.

185 Mnaona, msijali kuhusu Urusi. Urusi ni kokoto ndogo pwani. Msihofu kuhusu ukomunisti. Wewe angalia mfumo wa Urumi, wakati unapounganika na makanisa. Hakuna kitu kilichoandikwa katika Maandiko kuhusu ukomunisti kutawala ulimwengu.

Nami ninafuata Neno, haidhuru kitu kingine chochote kinaenda wapi. Ni Neno ninaloliamini. Mfumo wa Urumi ndio unaouchukua ulimwengu. Nao mfumo wa Urumi ndio mama wa madhehebu. Hakujawa kamwe na madhehebu yo yote mpaka Rumi, na kila moja yao yalitoka kwake. Na Biblia ilisema hivyo, "Yeye alikuwa mama wa makahaba." Ningeweza kukaa nusu siku juu ya jambo hilo, tena, lakini nadhani afadhali niendeleo.

186 Wakati adui anapotushambulia, basi, "Loo, nakwambia, unapaswa kuja kujiunga na ..." Utafanya nini, kurudi nyuma, kupatana? Si askari halisi, hatafanya hivyo. La, bwana.

Tunafanya nini basi? Akili, "Iweni na nia ile iliyokuwa katika Kristo ..." Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] "Nia iliyokuwa ndani ya Kristo, iwe pamoja nawe." Alikuwa na nia ya namna gani? Dumu na Neno. Hiyo ni kweli. Alidumu katika Neno, Neno la Baba, ndipo akamshinda adui kila wakati. Sasa, wakati adui anashambulia na kujaribu kusema yakupasa kutenda *hili* na kufanya *lile*, utafanyaje? Dumu na Neno. Hiyo ni kweli.

187 Unataka kufanya nini basi? Chukua Neno. Neno ni nini? Biblia ilisema hapa. Tunalisoma tu. Kwa kuwa Roho, na wa Mungu, ni Neno. Mnaona? Angalia hapa. "Na chukueni chapeo ya wokovu, na Upanga, Upanga wa Roho." Upanga wa Roho! Nini? Roho anayeingia kupitia kwa nia yako na kuingia ndani yako, na Upanga wa Roho huyo ni Neno la Mungu.

Roho huyo anapigana na kitu gani? Roho Mtakatifu anapigana na nini, mihemuko, hisia? [Kusanyiko linasema, "Neno." — Mh.] Neno; moyo! Whiu! Utukufu! Inapigana na kitu gani, kujisikia? Neno! Neno! Hebu tuseme jambo hilo, Neno! ["Neno!"] Neno! ["Neno!"] Neno la Mungu ndilo Roho hupigana kwalo.

Roho wa Mungu anamwendea Ibilisi moja kwa moja, na kusema, "Imeandikwa!" Amina! "Imeandikwa!" Ndipo ibilisi anaondoka.

188 Tunafanya nini? Kuchukua Upanga, ambao ni Neno la Mungu, tunauchomoa Huo kwa kutumia (nini?) mkono wa imani, mkono wenye nguvu wa imani, Upanga ukatao kuwili. Biblia ilisema katika Waebrania 4, "Ni—Ni Upanga ukatao kuwili," hukata pande zote mbili ukija na ukienda.

Ndugu, anafanya nini? Chukua Neno. Mchukue Roho, acha Roho aingie moyoni mwako. Fungua nia yako, useme, "Neno Lako ni kweli." Sasa, fanya hivi, dada. [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] "Neno Lako ni kweli."

"Bwana, sitajali jinsi ninavyojisikia, yale mtu ye yote, anayosema mwenyewe. Ninafunga, ninasafisha kila moja ya njia zangu, mahangaiko yote, na mashaka, na kutokuamini ambako nimepata kuwa nako. Kila kuhisi ulikowahi kuwa nako, maradhi yote niliyowahi kuwa nayo, kila kitu kingine nilichopata kuwa nacho, ninavitupilia vyote nje. Ninavipuuza vyote. Ninakuja moja kwa moja kwa Roho yangu. Ee Bwana, shuka chini. Ulisema ulinifanya kuwa na uhuru wa kuchagua."

"Wewe ni, Mwanangu."

189 "Vema, nafungua moyo wangu na akili yangu. Njoo, Bwana Yesu."

Na ushike Imani, huo Upanga wa Roho, BWANA ASEMA HIVI. Piga kelele, "Haleluya!" Amina. Kisha ukate kila adui aliye mbele yako. Amina. Hilo hapo. Mkate kila adui. Iwapo pe—pepo mchafu wa kale anakufanya ujisikie... Katilia mbali kitu hicho kwa Neno la Bwana.

Nguvu yetu, ni, "Furaha ya Bwana ndiyo nguvu yangu."

190 "Ondoka kwangu." Piga makelele! Umkate kwa Neno. Iwe ni pepo, iwe ni adui, iwe ni maradhi, iwe ni ugonjwa, cho chote kile, chukua hilo Neno ulivute kwa Upanga. Na kama ukilipiga dharuba mara ya kwanza, nalo halielekei kusogea, lipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena. Na ulipige dharuba mpaka umetoboa tundu, kama kifaranga mdogo akijitokeza mwenyewe nje; ama tai, ndivyo ulivyo. Jitokeze moja kwa moja kutoka hilo gamba la kale la maradhi. Fyeka upate njia ya kutokea, kisha useme, "Haleluya! Yuko wapi mwingine?" Amina. Hiyo ndiyo vita. Huyu ni askari. Huyu ni askari wa msalaba. Naam, bwana. Mtupilie nje kila adui.

191 Kwa nini? Kwa nini? Sisi, Uzao wa kifalme wa Ibrahimu uliochaguliwa tangu zamani. Wakati Ibrahimu alipokataa kila kitu ambacho kilikuwa ni kinyume cha Neno la Mungu, alikata njia yake moja kwa moja kupitia kila kizuizi kilichokuja mbele yake. Wakasema, "Mke wako ni mzee sana." Yeye alikikata tu kitu hicho njiani. Ibilisi alisema, "Huwezi kutenda jambo *hili*. Huwezi kutenda *lile*." Ibrahimu alikikata akakitupilia mbali. Alikipiga dharuba, akakipiga dharuba, mpaka akajitoa.

"Wapi mwingine, Bwana?"

"Sogea hema yako *hapa* juu." Yeye alipanda akaenda akamjengea madhabahu kule.

Akaenda kule, ndipo Shetani akaja, akasema, "Sasa, nitakwambia, hapa si mahali pazuri."

"Nitakaa papa hapa. Ondoka kwenye uwanja wangu." Akasema, "Haleluya!"

Lutu akasema, "Afadhali uje huku chini. Tuna wakati mzuri hapa chini. Sote tuna madhehebu yetu hapa chini. Naam, mke wangu ni mkubwa wa shirika la waandishi na kadhalika, humu mjini. Nawaambia, mnapaswa kushuka kuja hapa."

Sara akasema, "Ibrahimu ..."

192 "Nyamaza, Sara." Haleluya! "Simama papa hapa. Hapa ndipo Mungu aliponiweka. Papa hapa ndipo ninaposimama."

Hapa ndipo Mungu aliponiweka.

Wote wasifu nguvu za Jina la Yesu!

Hebu kusujudu kwa Malaika kushuke;

Kuleta taji ya kifalme,

Na kumvika taji kuwa Bwana wa wote.

Juu ya Kristo, Mwamba imara, nasimama;

Mahali pengine pote ni mchanga udidimiao,

Sehemu zingine zote ni mchanga udidimiao.

Hata mauti yenyewe, cho chote kile, ni mchanga udidimiao. Kwake Kristo, Mwamba imara, nasimama.

193 "Uzao wa kifalme wa Ibrahimu." Ule Uzao wa kifalme! Naam, jeshi la Uingereza lililochaguliwa vizuri sana ni jamii ya kifalme ya Uingereza, damu ya kifalme, kila kitu. Na Uzao wa kifalme wa Kristo ni Kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu, limejazwa na Roho Mtakatifu. Nini? Uzao wa Kifalme, kwa ahadi, si kwa mihemuko. Lakini, kwa ahadi ya Mungu, wanasimama na Neno la Mungu, na kukata njia yao ingawaje, wakipaza sauti, "Haleluya!"

Hata mauti huja na kusema, "Inakunyemelea kifichifichi."

Sema, "Toa njia, Yordani, ninavuka." Ninavuka." Fyeka upate njia ya kuingilia, Nchi ya Ahadi. Amina.

194 Inakuwaje wakati vita vimekwisha? Ninafunga sasa, hakika kabisa. Wakati vita vimekwisha, na watakatifu wanakuja wakienda Nyumbani, nataka kuwaulizeni jambo fulani, ni kitu gani kilichotukia?

Ilikuwa wakati Hitler alipoingia Ufaransa? Mbona, walisema hata usingeweza kuona mbingu, kwa kitambo kidogo, kwa ajili ya ndege zote. Wajerumani walipiga hatua kikakamavu kabisa. [Ndugu Branham anapanda jukwaani mara mbili — Mh.] Mnaona, walikuwa wamesimama, wakipita, wakishangilia ushindi.

Stalin alipokuja Urusi, kwa maili nyingi kule nyuma, kila kifarua nyuma kidogo tu ya kingine, aliushambulia tu Berlin kwa mizinga hata hamna kilichosalia. Hivyo tu. Na wakati walipokwenda, na hawa Wajerumani ... Hawa askari wa Kirusi wakisherehekea, waliingia na hilo, mwajua, jambo hilo dogo la kuchekesha wanalofanya. Niliiona kwenye picha, wakati mmoja huko London, jinsi walivyoingia, ile picha halisi ya kitu kile, kile kilichotukia, wakiingia, wakisherehekea. Loo, jamani!

195 Tuliposikia ya kwamba vita vimekwisha, tulipiga makelele, tukapiga filimbi. Wakati shujaa aliporudi, tulikutana nao kule juu. Walipaza sauti. Walipiga makelele. Nilikuwa na binamu aliyekuwa mle ndani, kasema, aliporudi, wote wa kale ... Wale mashujaa wa zamani walikuwa wamejaa majeraha sana, hata hawangeweza kutoka kitandani, kwa hiyo waliwavingirisha tu juu ya meli walipoingia, ili kuona ile Sanamu ya Uhuru imesimama. Kasema, "Hao watu mashuhuri wakisimama pale, wanalia tu, na kuanguka moja kwa moja namna *hiyo*, walipoona ile Sanamu ya Uhuru." Wameodoka nyumbani miaka minne wakipigana, wametiwa kihoro, na vita na kadhalika. Lakini walijua kwamba mke, na mpenzi wa moyo, na mama, na baba, na watoto, na yote waliyopenda yako nyuma ya ile Sanamu ya Uhuru. Iliwakilisha walichokuwa wakipigania. Loo, filimbi zililia, na New York ikaingia kwenye vigelegele, hivyo tu, wakati mashujaa wao walikuja wanapiga hatua za taratibu. Hilo litakuwa ni jambo dogo.

196 Wakati mmoja wakati Kaisari, baada ya vita vikuu, alisema, "Ninataka shujaa wangu mashuhuri sana apande nami katika sherehe hii kuu ya ushindi juu ya adui yetu." Na kila mmoja wa maofisa alitengeneza mapambo yao ya manyoya, na wakang'arisha ngao zao, na wakapita taratibu, unajua, namna hiyo, kama —kama askari halisi namna hiyo. Baada ya kitambo kidogo, maskini mzee mmoja akaja, akakata. Jamani! Yeye kwa namna fulani aliangalia juu, na kuanza, namna *hiyo*. Kaisari akasema, "Ngoja kidogo. Ngoja kidogo. Wewe," hata hujavaa kama ma—maafisa, kasema, "njoo hapa." Kasema, "Ulipata wapi makovu hayo?"

Akasema, "Huko nje kwenye uwanja wa vita."

Kasema, "Panda hapa juu. Wewe ndiye mtu ninayetaka kumweka karibu nami." Kwa nini? Alionesha ya kwamba alikuwa vitani.

Loo, Mungu amrehemu mtu anayeweza kukata mkono wake kwenye kopo la samaki wa sadini na apate kupewa hongera. Nataka nipate makovu ya vita. Kama vile Paulo alivyosema, "Ninachukua mwilini mwangu alama za Yesu Kristo." Hiyo ndiyo sababu ninataka kupigana uwanjani.

197 Siku moja, wakati Kapteni wetu Mkuu atakapokuja, Ambaye alituvulisha silaha, aliyetupa silaha za Mungu, Roho Mtakatifu akatupa Neno Lake la kupigania, kusimama nje huko; wakati Kapteni wetu Mkuu atakapokuja, nataka kupanda kwenye gari niende nyumbani pamoja Naye. Na wewe je? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Basi, nimshikapo maskini mke wangu mkono, ninaangalia hapa na kuwaona ndugu zangu na wake zao, na watoto wao, tutakapoanza kutembea tukishuka zile paradiso za Mungu, na Malaika wakijaza hewa kwa nyimbo, juu namna hiyo; nena kuhusu kusherehekea!

Na wakati vita vitakapokwisha, tutavaa taji. Loo, jamani! Loo, askari wa msalaba, asubuhi ya leo, vuta mkono huo wa imani hapa nje, na ushikilie Silaha hii.

Vipi kuhusu hilo, dada, uko tayari? [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] Vuta Silaha hiyo, useme, "Mungu, sijali nini—kile Ibilisi ameniambia, ni kiasi gani mtu mwingine yeyote amesema. Asubuhi ya leo, ninaamini." [Huyo dada anasema, "Ninaamini, pia."] "Ninaamini."

198 Kama nilivyosema hivi majuzi, kidogo ... Ninaamini Jumapili chache zilizopita, kulikuwa na mtu aliyetoa ndoto. Yeye aliota ya kwamba ibilisi alikuwa ni mtoto mdogo sana, alimkimbilia. Akasema, "Buu!" Naye akaruka nyuma kisha ibilisi akaanza kuwa mkubwa zaidi. "Buu!" Naye akaruka nyuma, kisha huyo ibilisi

akawa mkubwa na mkubwa. Hatimaye ibilisi akawa mkubwa kama yeye, na angemshinda. Alijua ilibidi apigane naye kwa kitu fulani, kwa hiyo akaangalia kote. Hakuweza kupata kitu cha kupigana naye. Yeye aliichukua tu Biblia. Ndipo ibilisi akasema, "Buu!" Naye akasema, "Buu!" kwake moja kwa moja, ndipo ibilisi akaanza kuwa mdogo zaidi, na mdogo zaidi, na mdogo zaidi. Na, hatimaye, akampiga akamuua kwa Neno.

199 Wewe ni askari, sivyo, dada? [Ndugu Branham tena anazungumza na yule dada mgonjwa — Mh.] Chukua Neno hilo na useme, "Imeandikwa." Amina. "Sitakufa. Nitaishi. Nitaketi moja kwa moja katika maskani hii na kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake, pamoja na hao wengine."

Mnaamini jambo hilo, watakatifu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Amina.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

200 Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, jalia ijulikane leo ya kwamba Wewe ungali Mungu. Haidhuru ningehubiri kiasi gani, ningesema mambo mangapi, Bwana, Neno kutoka Kwako linatosha.

Hizi lesu zimewekwa hapa, zikiwakilisha wagonjwa. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba baraka Zako na nguvu zitakaa juu ya kila mmoja wao, ninapoweka mikono yangu juu ya hizo. Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utazitia mafuta lesu hizi kwa Uwepo Wako mtakatifu, kwa kuwa zimeandikwa katika Neno. Si kitu dhidi ya Neno. Lakini ilisemwa katika Neno, ya kwamba, "Walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo, lesu na nguo. Pepo wachafu waliwatoka watu, nao wakaponywa magonjwa mbalimbali." Sasa, sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe bado ni Mungu, na Wewe ungali Roho Mtakatifu yeye yule. Ninaweka mikono yangu juu ya lesu hizi, katika Jina la Bwana Yesu, na kuomba ya kwamba Wewe umbariki na kumponya kila mmoja wao.

201 Ee Mungu, huyu anayelala hapa kwenye kitanda, ambaye amekuwa hapa, ni mtoto tu, maskini msichana mdogo mzuri. Hawezi kuishi, Bwana. Shetani amemtendea maovu. Na madaktari wapendwa wa dunia hii wamejaribu sana, hapana shaka, kumwokoia mtoto huyo. Hawawezi kamwe kufanya hivyo. Wako mwisho wa akili zao. Hawajui kitu kingine cha kufanya. Lakini, Bwana, nina furaha sana ya kwamba kuna sura nyingine iliyoandikwa. Tunaweza kufungua ukurasa mwingine, na katika ukurasa huu tunaona Tabibu Mkuu akiingia. Tunamwita Yeye apate kutushauri asubuhi hii.

202 Sasa, Bwana, je! haikuandikwa hapa katika Neno Lako, kwamba "ishara hizi zitafuatana na hao wanaoamini"? Bwana, kama mimi si mwamini, nifanye mmoja sasa. Kama msichana huyu mdogo si mwamini, mfanye mwaminio sasa. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Imeandikwa pia, "Katika Jina Langu watatoa pepo." Bwana, hayo—hayo ni Maneno Yako. Ni Yako. Ni Neno Lako. Na sasa kama mtumishi Wako ...

Kama Wewe ulivyosema, "Wakiwapo wawili au watatu kati yenu wamekutanika pamoja, nitakuwa miongoni mwenu; na kama mtapatana, katika kitu kimoja, na kuomba, mtakipokea."

203 Mungu, mtoto huyu labda ndiye mtu aliye mgonjwa kuliko wote jengoni asubuhi hii, kwa sababu hawezi kuishi bila Wewe, muda mrefu zaidi, naye ndiye mgonjwa sana. Kwa hiyo, sisi sote, tunakubaliana, kama kila askari anayesimama hapa. Na katika kundi hili unasimama Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

Tunasogea kumkabili Shetani sasa. Afadhali ujitayarisha kwenda, Shetani, sababu silaha zetu zinametameta, bendera zinapepea, wanaume na wanawake wanashika mapanga, wakipiga hatua mbele sasa kupambana nawe kwa ajili ya msichana huyu mdogo. Toka ndani yake, Shetani. Mwache mtoto huyo. Sisi tukiwa Jeshi la Mungu aliye hai, tunakukataa! Mwache, katika Jina la Yesu Kristo.

204 Ninaenda kumwekea mikono. Na, Shetani, umemfunga mtoto huyu, umefanya uovu huu. Ninajua ya kwamba wewe ni zaidi ya mshindani wa mwanadamu, bali wewe hushindani na Bwana wangu, kwa hiyo ninakuja katika Jina Lake. Mwache, ewe roho wa ibilisi. Ewe pepo wa magonjwa, toka kwa mtoto huyu, na jalia aende huru, tangu leo na kuendelea. Ninatamka jambo hili, katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa, Bwana Mungu, Wewe uliyewafufua wafu na kuthibitisha ya kwamba Wewe ulikuwa Mungu, mfufue mwanamke huyu kijana kwa afya yake na nguvu zake tena, kwamba atasimama katika jengo hili hapa. Ibilisi amemwacha! ...?... atamponya. Jalia aishi kwa utukufu na heshima ya Mungu.

I—Imenenwa, sasa na itendeke.

205 Kuna wengine hapa wanaotaka kuinua mikono yenu na kusema, "Ninataka kuombewa. Mimi ni mgonjwa. Ninamhitaji Mungu"? Sijui tuna muda gani. Tuna wakati wa kutosha kuwaacha hao watu wapite hapa. Ninajisikia tu kufariji sana asubuhi ya leo sasa. Naam. Naam. Ninataka uje hapa chini, Billy, na uchukue tu labda sehemu hii moja papa hapa, upande *huu* hapa, peke yako. Hebu tu sehemu hii ije kwanza, ndipo tuchukue sehemu ya nyuma baada ya hapo, tu mpaka kwenye yale marefu ya kanisa kule. Ndipo tutawachukua namna hiyo, basi hawataniii ...

Na sasa ninataka Ndugu Neville na baadhi ya ndugu zangu wahudumu wasimame hapa karibu nami, papa hapa, ili mweze kuwapeleka moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa tena. Vema. Vema. Sasa mimi



...

206 Ni wangapi wenu wamevaa silaha zao? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

[Ndugu Branham anaondoka mimbarani na kuzungumza na dada ambaye alikuwa amemwomba — Mh.] Itakuwa tofauti sasa. Nenda nyumbani, uwe mzima sasa, uwe mzima.

Amina. Loo, jamani! Ninyi askari wote, vuteni Panga. Vuteni Upanga, askari wa msalaba, mkipiga hatua, mkipiga hatua.

Juu ya Kristo, Mwamba imara, nasimama.  
Ardhi nyingine yote ni mchanga unaodidimia.

207 Vema, njoni moja kwa moja, moja kwa moja upande huu *hapa*. Kila mtu katika maombi sasa, wanapopita.

Katika Jina la Yesu, mponye mwanamke huyu. Amina.

Vuta Upanga wako sasa. Endelea moja kwa moja kwenye kiti chako, ukipaza sauti.

[Ndugu Branham na wahudumu wanawaomba wagonjwa, mbali na maikrofoni, kwa sekunde arobaini na tano — Mh.]

Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia.

208 "Simile, Shetani!" Kuna nini, enyi askari? Hivi hamfikiri tunaweza kushinda? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina." — Mh.] Yeye tayari ameshindwa. Sisi ni zaidi ya washindi katika Kristo Yesu. Kila pepo alitupwa nje, kila kitu kingine. Amina.

Njoni hapa, ndugu zangu! ...?...

Ninaomba ya kwamba utamponya! ...?...

Mponye ndugu yangu, Doc; mponye, Baba, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye mama huyu. Njoo ...?...

Sasa, yeye alichukua ... Ilinibidi kuwauliza ndugu huko nyuma. Kila mahali, Bwana ...?

Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi! Ee Mungu, unajua kilicho moyoni mwake. Unajua yote kuhusu jambo hilo. Ninawaomba mama na baba. Katika Jina la Yesu Kristo, ninamsalimisha ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mimi ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mimi ...?...

Mungu, kuwa pamoja na dada yangu. Tunajua, miaka ilianza kuingia na kusababisha mauti kutaka kuushika mwili wa mwanamke. Sasa, katika Jina la Yesu ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mbariki msichana huyu mdogo, Bwana. Vita vyetu shuleni kule, ninajua yale anayopitia. Ninaomba utabariki. Jalia avute Upanga huo, asubuhi ya leo, na aende mbele! ...?... Mbariki mvulana huyu mdogo, Bwana; anakuja, akiliita Jina Lako, asubuhi ya leo; Ninaomba ya kwamba utaambatana na ...?...

Mungu, mbariki ndugu yangu, ukimjalia haja yake. Katika Jina la Bwana wetu Yesu, nililinena! ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba maombi haya.

Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba maombi haya.

Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba maombi haya.

Katika Jina la Yesu Kristo, sisi ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba maombi haya.

Katika Jina la Yesu Kristo ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

Katika Jina la Yesu Kristo!

[Mtu fulani anasema, "Baba alikufa." — Mh.] Mungu, msaidie, katika Jina la Yesu.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, sisi ...?...

Mungu, katika Jina la Yesu!

Katika Jina la Yesu Kristo ...?...

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu ...?...

Mnaelewa sasa?

Ee Mungu, jalia hili liondoke ...?

Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba! ...?... Jalia dada ...?...

209 Ee Mungu, ukimjua maskini mama huyo wa thamani, akipitia katika shida hii yote, naomba, Mungu, ya kwamba utaninii ...?... Juu yake.

Vuta Upanga huo, Ed, na usonge mbele, katika Jina la Yesu.

Ewe Mungu, mponye mwanamke yule. Jalia ombi lake. Jalia auchukue Upanga huo mbele zake, katika wakati wa shida.

Ee Mungu ...?... asubuhi hii. Ninaomba ya kwamba utaninii ...?...

Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu na kumpa afya. Na katika Jina la Yesu Kristo ...?...

Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, umpe afya, katika Jina la Yesu Kristo.

Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba unge—ungemponya ndugu yetu.

Mponye dada yetu, Bwana! ...?...

Baba, katika Jina la Yesu, mponye huyu, dada yetu, Baba.

Baba, ...?... Tunaomba katika Jina la Yesu. Mungu, mponye mwanamke huyu.

Ee Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe ...?...

Ee Mungu, mbariki, Baba! ...?... Jinsi tunavyowapenda hao jamaa wa kale, Bwana. Nami ninaomba ya kwamba utatimiza haja yake! ...?...

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba ndugu yangu ...?... Ee Mungu, ...?... Yeye, Ee Mungu ... askari wa msalaba. Naye atavuta Upanga huo, asubuhi ya leo, na kusonga mbele.

Mungu, sisi ...?... Jalia hili, Ee Bwana, ombi lake.

Mungu, mbariki ndugu ...?... Ninaomba ya kwamba utamponya, Bwana! ...?... Mpe shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo.

Ee Baba wa Mbinguni, maskini mhudumu huyu wa Injili, koo lake ...?... Ambapo ameosha katika vyungu ...?... Mungu, ninaomba ya kwamba utaninii ...?... Na wakati jeshi kuu la Mungu likiendelea mbele sasa, huku Upanga umeinuliwa, mpe ushindi, Bwana. Maskini mumewe hapa, Bwana, ambaye aliletwa kutoka kwenye kile kitanda cha kansa alikokuwa amelala, akifa kwa kansa, na madaktari wakimtoa, alipokuwa akienda. Naye yuko hapa, asubuhi ya leo, askari mdogo wa msalaba. Mtie nguvu, Bwana, kwa ajili ya huduma Yako, tunaomba, katika Jina la Yesu.

210 Ninamtaka maskini mama huyo ... Kuna kitu kingine na maskini mhubiri huyu hapa. Njoo hapa, Ndugu Kidd. Mtu huyu alirudishwa nyumbani kutoka hospitalini, hivi majuzi tu, akifa, akaliwa na kansa. [Dada Kidd anasema, "Mwaka mmoja uliopita." — Mh.] Mwaka mmoja uliopita. ["Miwili."] Miaka miwili iliyopita, kwa tezi dume. Daktari wake alimpa siku chache tu kuishi. Na asubuhi moja, tulikwenda kule, mapema

sana, tukamwomba, yule yule kama tu kwa ajili yenu, na hata hawawezi kupata dalili ya jambo hilo. [Kusanyiko linashangilia.] Alikuwa ameponywa. Amina. Yeye—yeye ... [Dada Kidd anasema, "Ilibidi nilikubali."] Yeye ana uzito zaidi sasa kuliko alivyowahi kuwa nao. Yeye na maskini mke wake wamekuwa katika kueneza Injili, labda kabla sijazaliwa. Yeye yupo hapa sasa ... [Ndugu Kidd anasema, "Miaka hamsini na mitano."] Miaka hamsini na mitano. Kabla hata sijaja duniani, walikuwa wakihubiri Injili. Na huyu hapa, ameponywa, akiwa na umri wa kama miaka sabini na mitano ama ... ["Themanini na moja."] Themanini na moja. [Ndugu Kidd anasema, "Tungekuwa na uamsho, mkutano wa majuma mawili, tuhubiri kila usiku."] Uamsho wa majuma mawili, tulifanya tu uamsho wa majuma mawili, na kuhubiri kila usiku. Akiwa na umri wa miaka themanini na moja, aliponywa, na kansa, wakati alipokuwa mzee.

211 Vema, dada, ni wakati wako sasa. Unaamini? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina." — Mh.] *Twendeni, Askari Wakristo*. Vema, dada. Ninyi, kwa kila mmoja wenu, tutafanya nini? BWANA ASEMA HIVI. Tunafanya nini, tunakaa hapa?

Shetani, umeshindwa. Tunakuja sasa. Tunapiga hatua kwenda kwenye Nchi ya ahadi. Ni kitu gani hicho? "Mlima huu ni nini, mbele ya Zerubabeli? Ni nani huyu, anayesimama mbele pale? Utakuwa tambarare." Kwa nini? Tukiwa na Upanga ukatao kuwili, tutamkatilia mbali kabisa. Hiyo ni kweli. Vema.

Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia;  
Kristo, Bwana wa kifalme,  
Huongoza dhidi ya adui; (akiwa na Neno Lake)  
Tukisonga mbele katika vita,  
Mnaona, bendera Zake zinaondoka!  
Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia.

212 Haleluya! Walifanya nini? Kitu kilichotangulia, vitani, kwa ajili ya Israeli, kitu kilichotangulia kilikuwa ni nini? Waimbaji walitangulia, kwanza. Ni nini kilichofuata? Sanduku. Kisha vita. Vema. Mnaamini jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Tutaimba *Twendeni, Askari wa Kikristo*. Tunaondoa kila shaka. Tukisimama kwa miguu yetu sasa, tunaenda vitani.

Hebu na tusimame sasa, kila mtu.  
Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia;  
Kristo, Bwana wa kifalme,  
Huongoza dhidi ya adui;

Tunamshindaje? Kwa Neno.  
Tunasonga mbele katika vita,  
Mnaona, bendera Yake inakwenda!  
Twendeni, askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia.  
Hatujagawanyika,  
Sote ni mwili mmoja;  
Mmoja katika tumaini na fundisho,  
Mmoja katika upendo.

213 Wote wanaoamini sasa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Haleluya! Unaamini hilo? ["Amina!"] Sisi ni washindi. Yuko wapi kila adui? Chini ya miguu yetu. Sisi ni nini leo? Tumefufuka katika Kristo!

Sasa, imekwisha, dada. [Ndugu Branham anazungumza tena na yule dada, aliyekuwa mgonjwa — Mh.] Unaamini jambo hilo? Nenda nyumbani sasa. Unajisikia sawa? Anasema anajisikia mzima sasa. Kila kitu ni sawa.

Ni wangapi huko nje wanaojisikia wazima? [Kusanyiko linashangilia kwa nguvu na kusema, "Amina." — Mh.] Nao walipopiga makelele, ukuta ulianguka, amina, nao wakautwaa. Amina. Waliuteka mji. Amina! Amina! Unamwamini? ["Amina."]

214 Sasa, msisahau ibada ya usiku wa leo. Ndugu Neville atakuwa hapa usiku wa leo, na kutuletea

ujumbe mzuri. Na Jumapili, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, kuwa hapa.

Sasa hebu na twendeni, huku tukisogea mbele. Na sasa, nje kutoka humu jengoni, hebu twendeni tukiimba *Twendeni, Askari*. Na tangu siku hii, na kuendelea, kamwe usitie Upanga huo kwenye ala tena. Uchomoe. Hebu na tushinde. "Wao walitoka, wakishinda, tena wapate kushinda." Vema, tena, kwenye kifungu hicho cha kwanza.

Twendeni askari Wakristo!  
Tukitembea kama kwenye vita,  
Pamoja na msalaba wa Yesu  
Ukitutangulia.



[www.messagehub.info](http://www.messagehub.info)

Mahubiri Na  
**William Marrion Branham**  
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7